

# MAISHA NI KUGHARIMIA

Mathias E. Mnyampala



MATHIAS E. MNYAMPALA

# *Maisha ni kugharimia*

DL2A – BULUU PUBLISHING

**DL2A – Buluu Publishing,**
**Shirika lisilo la faida (non-profit),**
**Nambari W942004818,**
**UFARANSA.**
**Barua-pepe : buluu.publishing@gmail.com**

**© MNYAMPALA 2013 (mswada na maandishi yake)**

**© DL2A – BULUU PUBLISHING 2013 (uhariri)**

**Kimehaririwa na Mathieu Roy.**

ISBN : 979-10-92789-02-7

**Haki zote zimehifadhiwa.**
**Sehemu yoyote ya kitabu hiki hairuhusiwi kuchapwa kwa njia yoyote ile iwe ya kimaandishi au kielektroni bila ya idhini ya wenye hakimiliki wenyewe.**



**MATHIAS E. MNYAMPALA (1917 – †1969)**

# *YALIYOMO*

YALIYOMO ........................................................................................ v

ZINDUO ........................................................................................ vii

DIBAJI ........................................................................................ xi

MAISHA NI KUGHARIMIA........................................................................ 1

UTANGULIZI ........................................................................................ 1

SURA YA KWANZA UTOTO WANGU ................................................ 4

SURA YA PILI KUHAMA NA MATOKEO YAKE ................................ 7

SURA YA TATU JANDO. MAMBO YA UJANA NA KUOA. ............... 11

SURA YA NNE KAZI YA UALIMU ....................................................... 14

SURA YA TANO MAENDELEO YA KAZI YA UALIMU .................... 18

SURA YA SITA MAENDELEO YA KAZI YA UKARANI .................... 21

SURA YA SABA KARANI WA KODI NA MAENDELEO MENGINE 24

SURA YA NANE MAENDELEO YA KAZI MANYONI NA MWISHO WA KAZI YANGU. NA MENGINEYO. ............................................... 29

SURA YA TISA MAKAO YA NYUMBANI – KAZI YA STOO NA NDOROBO. ........................................................................................ 34

SURA YA KUMI KARANI KATIKA PAULING & CO. LTD KONGWA NA MAREJEO KATIKA BOMA DODOMA. ....................................... 41

SURA YA KUMI NA MOJA KAZI YA KODI TENA NA MAENDELEO MENGI ........................................................................................ 44

SURA YA KUMI NA MBILI MAENDELEO YA KAZI YA HAZINA YA WENYEJI NA MATOKEO YAKE......................................................... 47

SURA YA KUMI NA TATU MAJUTO HUJA NYUMA........................ 53

SURA YA KUMI NA NNE KAZI UGENINI, NA KURUDI DODOMA 55

SURA YA KUMI NA TANO KARANI KATIKA IDARA YA WATER DEVELOPMENT DODOMA ....................................................................59

SURA YA KUMI NA SITA KARANI KATIKA IDARA YA KILIMO DODOMA..........................................................................................64

SURA YA KUMI NA SABA KAZI YA ULIWALI MPANDA................66

SURA YA KUMI NA NANE KUWA KADHI WA DAR ES SALAAM.67

SURA YA KUMI NA TISA KARII WA MAHAKAMA KUU ................68

PICHA NA VYETI VINGINE ....................................................................73

# *ZINDUO*

Marehemu Mathias E. Mnyampala aliandika habari za maisha yake wakati alipokuwa ameshaona kwamba anakomea mwisho wa uhai wake kutokana na kuumwa sana na ndwele miaka 1968-1969. Wakati huo alikuwa ameshakuza sana lugha ya Kiswahili kwa ufasaha wake wa kishairi na mambo mengine mengi pamoja yake vitabu vyake kuhusu historia ya Ugogo, siasa ya Ujamaa, dini na maisha ya wafu maarufu kama Mtemi Mazengo na Sheikh Kaluta Amri Abedi. Alikuwa mzalendo mkubwa wa Taifa la Tanzania na alijitolea kabisa kueneza lugha yake Kiswahili maisha yake yote. Mchango wake Mathias E. Mnyampala kwa fasihi ya Kiswahili na Taifa lake ni tukufu, kadiri ya kupewa heshima kubwa ya Nishani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Rais Ali Hassan Mwinyi mwaka 1994. Lakini kumbe dunia ya utafiti wa Vyuo Vikuu na ya biashara ya uhariri ilibakia muda mrefu sana uliozidi miaka arobaini katika ukosefu wa kumbukumbu na habari za mzungupule huyo wa Kiswahili.

Nilijaliwa kugundua mswada huo unaoitwa "*Maisha ni kugharimia*" mwaka 2007 mjini Dodoma pamoja na miswada mingi na nyaraka nyingine muhimu vilivyokuwa vinahifadhiwa kwa makini sana na mtoto wa pili wa mwandishi, Bwana Charles M. Mnyampala. Mtaalamu mkubwa wa Kiswahili, Profesa Mlinzi M. Mulozi aliyestaafu sasa kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alikuwa ameandika mwaka 1995 kwamba labda mtoto wa mwandishi anayo miswada ya baba yake na kuwa bado anaendelea kujaribu kuwasiliana na yeye.

Alikuwa amepata habari hiyo kutokana na uchunguzi wake kamili kuhusu historia ya ushairi wa Kiswahili uliomfikisha mara nyingi mjini Dodoma kwa Bi Mary Mangwela, mke wa marehemu Mathias E. Mnyampala. Lakini wakati huo Charles M. Mnyampala hakukaa mjini Dodoma. Alikuwa bado amesafiri katika sehemu mbalimbali na miswada hiyo kwa sababu ya uhamisho wa kazi yake katika Jeshi la Polisi la Tanzania.

Nilipoanza utafiti wangu kwa ajili ya kuandika tasnifu ya Udaktari kuhusu ushairi wa Mathias E. Mnyampala na ujenzi wa Taifa la Tanzania nilikutana na Profesa Mulokozi jijini Dar es Salaam. Kwa sababu ya wema wake nilipata shauri ya kwenda Dodoma kwa Bi Mary Mangwela kufahamu zaidi juu ya mume wake. Nilisafiri nikafanikiwa kukutana na Bi Mangwela na mtoto wake Bwana Charles M. Mnyampala aliyekuwa amerudi nyumbani kustaafu.

Bwana Charles M. Mnyampala alinipa heshima kubwa ya kuniamini wakati mimi ni mgeni aliyekuja kwa mara ya kwanza kwake akanionyesha mswada huo unaoitwa "*Maisha ni kugharimia"* na miswada mingine baada ya maelezo yangu kuhusu mpango wangu wa Udaktari. Wakati huo nilikuwa nimefurahi sana kwa sababu ya baraka hii maalum iliyokuwa inaathiri vizuri mno maendeleo ya kazi yangu ya utafiti. Pia nilikuwa ninaona kwamba miswada hiyo ni hazina kubwa upande wa historia ya fasihi ya Kiswahili na historia ya Tanzania, kama hazina ya Taifa la Tanzania. Nilimwarifu mara moja Profesa Mulokozi kuhusu ugunduzi wangu nikimwamini sana kama mwenye uwezo wa kuendeleza mambo hayo zaidi nikiwa ninakubaliana na Bwana Charles M. Mnyampala kupiga picha za kielektroni za miswada yote kwa ajili ya utafiti wangu na mpango mwingine wa uhifadhi wa kudumu.

Kanzi ya Mathias E. Mnyampala inawapa watafiti na wasomaji uwezo wa pekee wa kugundua miswada mingi ambayo haijachapishwa. Ilikuwa vigumu sana kupiga chapa zamani kwa sababu za taratibu na vikwazo vingi katika makampuni mbalimbali ya uchapishaji na gharama zake. Sasa hivi mwaka 2013 tunahudhuria mapinduzi ya kweli kwenye upande wa uhariri kwa sababu za maendeleo ya mtandao na kompyuta. Kwenye zama zetu za kiteknolojia na utandawazi shida si kupiga chapa tena, lugha yoyote iwe. Bali sharti uwe na uhodari wa akili pamoja na ufasaha wa lugha na bado mwandishi wa zamani kama Hayati Mathias E. Mnyampala anazo fikira njema nyingi kuwatanabahisha wasomaji na vijana wa kisasa. La kwanza wasishindwe na wasikate tamaa kabla ya kujaribu jaribu na jaribu tena mpaka wafanikiwe kabisa au kadiri yake kama yeye mwenyewe alifanikiwa kutoka utoto wake katika machunga ya Ugogo, bila kujua kusoma wala kuandika hadi umri wa kuoa mke na kulipa kodi, mpaka ubingwa wa lugha ya Kiswahili na utungaji wa idadi ya vitabu inayozidi ishirini na tano akiwa anadhaniwa na wataalamu wa ushairi wa Kiswahili na washairi wenzake wenyewe kuwa malenga mmoja mkuu wa Karne iliyopita.

Bwana Charles M. Mnyampala alikubali kupiga chapa ya mswada huo wa *Maisha ni kugharimia* kwa mara ya kwanza katika shirika lisilo la faida la Buluu Publishing. Shirika hilo linashughulika kuhariri vitabu nadra vinavyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili, lugha ya Afrika au tafsiri zake katika lugha nyingine mbalimbali pamoja na historia ya fasihi. Ni mswada wa pili ambao haujachapishwa kutolewa sasa baada ya kitabu cha *Historia ya Hayati Sheikh Kaluta Amri Abedi (1924-1964)* kilichochapishwa na Ahmadiyya Press mwaka 2011.

Ni tumaini langu kuwa vitabu vingine vitatolewa baada yake. Ninamshukuru sana Bwana Charles M. Mnyampala kwa kazi yake adimu ya kuhifadhi miswada ya Mathias E. Mnyampala kutoka miaka hiyo mingi na kugawa hazina yake na sisi wapenzi wa Kiswahili.

Mathieu ROY (mtafiti, mhariri)

22 Julai 2013

Paris, UFARANSA

Barua-Pepe: mathieu.roy.eu@gmail.com

# *DIBAJI*

Tangu kale historia za watu maarufu zilihifadhiwa na vizazi kwa njia za maandishi au masimulizi ya midomo tu kwa kadiri ya mtu mwenyewe alivyokuwa. Nikiwa ni mtoto wa pili kati ya watoto watatu wa Hayati Mathias Eugen Mnyampala ambaye alikuwa mwandishi wa kifasihi, ninayo furaha kubwa kuweka mbele ya wasomaji watukufu kitabu hiki cha historia hii kutokana na maandishi yake ambayo katika uhai wake kila tukio kwa mkono wake akiandika hadi mwisho wa uhai wake. Kama alivyoandika katika utangulizi wa kitabu hiki kinachoitwa "*Maisha ni kugharimia*" ni kwamba hakupata bahati ya kupelekwa shuleni bali alijitahidi kujisomesha hadi akawa bingwa sawa na wale waliopelekwa shuleni. Kwa hiyo maisha yake aliyagharimikia sana katika uhai wake wote.

Hayati Mathias Eugen Mnyampala licha ya mswada wa kitabu hiki pia aliandika miswada ifuatayo ambayo hadi leo haijachapishwa nayo ni:-

1. UGOGO NA ARDHI YAKE
2. MASHAIRI YA VIDATO
3. MAHADHI YA KISWAHILI
4. AZIMIO LA ARUSHA NA MAANDIKO MATAKATIFU
5. UFASAHA WA KISWAHILI
6. HAZINA YA WASHAIRI
7. MAISHA YA MTEMI MAZENGO

Lakini kuna miswada yake mingine ninayokuwa nayo iliyowahi kuchapishwa katika sura nzuri ya vitabu wakati angali hai. Vitabu hivyo vinapatikana tena au la.

Orodha yao ni kama ifuatayo:-

1. DIWANI YA LAMBERT (iliyesahihishwa na kuhaririwa na Mathias E. Mnyampala)
2. WAADHI WA USHAIRI
3. UTENZI WA ENJILI
4. DIWANI YA MNYAMPALA
5. NGONJERA ZA UKUTA I
6. NGONJERA ZA UKUTA II
7. KISA CHA MRINA ASALI NA WENZAKE WAWILI
8. MBINU ZA UJAMAA
9. UTENZI WA ZABURI
10. HISTORIA, MILA NA DESTURI ZA WAGOGO WA TANGANYIKA
11. KITO CHA HEKIMA I
12. KITO CHA HEKIMA II
13. FASILI JOHARI YA MASHAIRI
14. MASHAIRI YA HEKIMA NA MALUMBANO YA USHAIRI
15. TAALUMA YA KISWAHILI
16. HISTORIA YA HAYATI SHEIKH KALUTA AMRI ABEDI

Kwa sababu moja au nyingine yale mashirika yaliyokuwa yamechapisha miswada ya Hayati Mzee Mnyampala yalisitisha kazi hiyo na matokeo yake ni kwamba miswada aliyoiacha haijachapishwa hadi sasa na vile vitabu vilivyochapishwa wakati angali hai havijachapishwa kwa matoleo mengine na hivyo havipatikani kirahisi.

Baada ya kifo chake Hayati Mathias Eugen Mnyampala, miswada niliyoitaja hapo juu kuwa mikononi mwangu nilianza juhudi za kuyafikia makampuni mbalimbali ya hapa nchini ili waweze kuchapisha lakini hadi leo imeshindikana bila sababu za kuridhisha.

Mnamo mwezi wa pili 2007 alinifikia Mathieu Roy toka Ufaransa kwa ajili ya kufanya utafiti juu ya maisha ya Hayati Mathias E. Mnyampala. Bwana Mathieu Roy amekuwa nami kati ya mwaka huo 2007 hadi 2012, katika utafiti amefanikiwa kutunukiwa shahada ya Udaktari (PhD) na ndiye aliyenipa njia ya kitabu hiki kichapwe.

Mheshimiwa Hayati Mathias E. Mnyampala alisifika kwa kuanzisha mitindo[1] ifuatayo ya mashairi:-

MTINDO WA MASHAIRI YA MTIRIRIKO: “Mtindo wa namna hiyo humtaka mshairi ambaye ni tajiri wa misamiati wa Kiswahili ili asitindikiwe na urari wa vina”. Katika kitabu chake cha *Diwani ya Mnyampala* alitunga shairi akisema:-

**TUNGENI MTIRIRIKO**

Mhariri mhabubu, pokea wangu mwandiko,

Napenda kuwa hotubu, washairi walioko,

Si kama nawaghilibu, na kujitia vituko,

Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

[1] Kuhusu miundo na arudhi vya ushairi wa Mathias E. Mnyampala, *Taz*. k. 323 – 729 na k. 799 – 946 katika uchunguzi ufuatao (Kifaransa) :
Roy, Mathieu. *MATHIAS E. MNYAMPALA (1917-1969): POÉSIE D'EXPRESSION SWAHILIE ET CONSTRUCTION NATIONALE TANZANIENNE.* Diss. Institut National des Langues et Civilisations Orientales-INALCO PARIS-LANGUES O', 2013.
http://tel.archives-ouvertes.fr/tel-00778667

Msichukue ghadhabu, kwa mabavu na vituko.
Chungulie taratibu, usanifu beti zako,
Kama wajibu jawabu, ukae kwanza kitako,
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Nisikie Masharubu, wape habari wa Keko,
Mwingine sikughilibu, na vingine lisiweko,
Sitoke kwenye kilabu, ukajidai mwandiko,
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Uliza kwanza swahibu, umwendee kwa kicheko,
Pekee taliharibu, likose hata mwitiko,
Bali wepuke kidhabu, huyo awe sumu kwako,
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Kisa kilichokusibu, kipate nacho mwandiko,
Maanaye na sababu, mwanzo ni chokochoko,
Ni kipawa cha Wahabu, usipate masumbuko,
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Mwendo huo siharibu, vinginevyo lisiweko,
Ukianza na Hatibu, simwite tena Maiko,

Na uzuri wa dhahabu, sitie mchanganyiko,
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Tungozo ziwe dhahabu, zambatane na mwitiko,
Wengi wasitaajabu, jinsi ya mtiririko,
Liimbwapo ni taibu, lipendeze walioko,
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Asiliye ughaibu, moyoni ndilo chimbuko,
Yaliimbwa na mababu, hao waliokuweko,
Hawakulewa sharabu, waliotunza tambiko,
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Walotunga ya thawabu, na matusi yasiweko,
Watunzaji wa madhehebu, na dini na zilizoko,
Kumtukuza Wahabu, majambo mtakasiko,
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Beti kumi kwa hesabu, hazina mchanganyiko,
Nimemuweka Katibu, hapo kakaa kitako,
Kati 'bu' imeratibu, mwisho 'ko' imekuweko,
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

MTINDO WA MASHAIRI YA MSISITIZO: Alianzisha utungaji wa mashairi kwa msisitizo. Kila ubeti ulikuwa na kipande cha kusisitiza maudhui yaliyotengwa katika ubeti huo. Pia katika kitabu chake cha Diwani ya Mnyampala alitunga shairi akisema:-

NATUNGA **MSISITIZO**

Nawapangia maneno, ya sifa na walekezo,
Na kuzitoa mifano, zinase nyoyo mawazo,
Usemi wa sisitizo;
Sisitizo mlingano, usioleta mivizo,
Maagizo yawe **manono,** nayatilia mkazo,
Natunga masisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Tutunge ya tangamano, wana wapewe agizo,
Tuwafunze maagano, yasiyoleta chagizo,
Maovu kuwa katazo;
Katazo la matukano, yanayoleta mzozo,
Zogo halina **patano,** mbele lina maapizo,
Natunga msisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Utungo una mkono, wa kheri na matulizo,
Matulizo ya mtuno, usioleta vikwazo,
Ni mema matangulizo;
Tangulizo la maono, kwani una bembelezo,
Watu waache **kinzano,** kwani huleta tatizo,
Natunga msisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Tungo hizi kama ngano, kwa mkulima pendezo,
Hung'aa katika chano, makapi hata masazo,
Katu hazina chukizo,
Chukizo la baya pano, unaoleta ufyozo,
Bali ni **maridhiano,** ubani leta chetezo,
Natunga msisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Shikamaneni mikono, epukeni angamizo,
Tuepuke mapambano, maneno ya mkwaruzo,
Si maungwana utwezo;
Utwezo wa maumano, uadui pandikizo,
Cheka muonyeshe **meno,** siwe kama hatunazo,
Natunga msisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Zifanyeni mikutano, machungu mtie pozo,
Mema yale mashindano, kati hayana katazo,
Bali neno la umizo;
Umizo lenye mibano, kudhani kama mchezo,
Akheri **uhusiano,** tuepuke magombezo,
Natunga msisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Tafuteni mapendano, kuepuka ubwakizo,
Si vibaya makanyano, kwa wale wenye puuzo,
Tusilete magombezo;
Magombezo yele mno, na matusi mzo mzo,
Huvunja **shirikiano,** bagukano na utwezo,
Natunga msisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Vuteni sikilizano, ziada yenu ni tuzo,
Tuzo la ujulikano, mwororo uso vikwazo,
Muepuke ambukizo;
Ambukizo la mang'ano, magomvi na mapaazo,
Tungeacha **matetano**, tutunge tungo zijazo,
Natunga msisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Nashona mpya mshono, gazetini ni pambizo,
Tungo za uwezekano, kama wa nyumba na nguzo,
Kwa wagonjwa ni uguzo;
Uguzo dawa ya mbono, isiyokuwa na tozo,
Tungo mistari **tano**; wa sita ni mwishilizo,
Natunga msisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Si tungo za msumeno, kukwaruza kwa kerezo,
Khamis kasifu mno, mng'ao wa suko kwazo,
Zinacho kielelezo,
Kielelezo fatano, wa kupata elekezo,
Kisoma watoa **jino**, acha zipate enezo,
Natunga msisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

MTINDO WA MASHAIRI YA NGONJERA: Alifufua na kuendeleza sanaa na utunzi wa mashairi ya neno ngonjera. Ngonjera ni neno la asili ya Kigogo lenye maana ya kwenda pamoja. Ni mashairi yaliyovuma sana wakati wa siasa ya Ujamaa. Ambapo watu walitakiwa kuwa pamoja, kuishi pamoja katika vijiji vya ujamaa ili kushirikiana katika ujenzi wa Taifa na kula matunda ya Taifa pamoja. Mashairi hayo katika kitabu cha *Ngonjera za UKUTA, Kitabu cha Kwanza,* alitunga shairi akisema:-

**NGONJERA NI KITU GANI**

Watu wengi huuliza, “Ni nini maana ya ngonjera?

Hivyo, kable ya kuendelea na mashairi haya ya ngojera

Na vidokezo vyake, ninaanza kwa kulijibu swali hilo:

MDADISI

Ngonjera ni kitu gani, nasikia kila mara
Yatamkwa midomoni, tena mbele ya hadhara
Je maana yake nini, nami nipate busara
Maana yake ngonjera, nambie nami nijue

JAWABU

Ngonjera zina kiini, cha mafunzo ya busara,
Mafunzo yenye kipini, cha kuamsha fikira
Za mawazo akilini, na kugeuza majira
Maana yake ngonjera, ni mafunzo kwa shairi

MDADISI

Ni mafunzo yapi hayo; ya hekima na ubora?
Yatiayo watu moyo, kwa jitihada na ghera
Ufanisi yaletayo, ya kugeuza majira
Maana yake ngonjera, nambie nami nijue

JAWABU

Mafunzo yatolewayo, kwa usemi wa hadhara
Mema yachangamshayo, kwa tabasamu ya sura
Ni ghibu itumikayo, kwa fikira na busara
Maana yake ngonjera, ni mafunzo kwa shairi.

MDADISI

Jaribu kunitajia, nami nipate yadara
Mbele yaje nifalia, yawe kwangu kama nira
Na nitambue dunia, nizinduke mimi jura
Maana yake ngonjera, niambie nami nijue

JAWABU

Ni mafunzo kwa jamia, Ujamaa kuudara
Siasa kuzingatia, tudhibiti barabara
Usawa kuufikia, tofauti ni hasara
Maana yake ngonjera, ni mafunzo kwa shairi.

MDADISI

Je nalo Azimio, lililogeuzwa sura
Lenye matumainio, la kuangusha wakora
Heri yake majilio, inaonyesha ishara?
Maana yake ngonjera, nambie nami nijue

JAWABU

La Arusha Azimio, mabepari lawapora
Waanguke mwangushio, wanahema kwa papara
Unyonyaji mwishilio, waisha bila subira
Maana yake ngonjera, ni mafunzo kwa shairi

MDADISI

Ngonjera kila mahala, wazitaja na kuchora
Zapendwa kama chakula, twache mbali msihara
Ngonjera zina muwala, za hekima si hasira
Maana yake ngonjera, nambie nami nijue

JAWABU

Kazileta Mnyampala, wa UKUTA kazichora
Ya siasa na muwala, ya busara na ubora
Hayana ndani shakala, ila ya njema fikira
Maana yake ngonjera, ni mafunzo kwa shairi

MTINDO WA MASHAIRI YA VIDATO: Alianzisha mtindo wa mashairi ya vidato. Katika mswada wake wa *Hazina ya washairi* ameelezea kuwa mtindo huo aliuanzisha mwaka wa 1966. Ukifanana kidogo na ule uitwao "msisitizo" kwa mawazo mazito na yenye hekima ya mzamo sana wa mashairi mazito. Alitunga shairi akisema:

**TUSISEME HATUWEZI, AWEZALO BIN ADAMU**

IKIWA nia hatuna, ya kufanya mazoezi,
Ya kufua na kusana, na kufanya sana kazi,
VIPI mambo yatafana, nasi tuwe wagunduzi?
TUSISEME "hatuwezi"; awezalo BINADAMU.

IKIWA wewe huwezi, waliwezaji wa ng'ambo?
Meli zina matembezi, baharini kwa mitambo,
VIPI sisi tuwe bozi, tushindwe madogo mambo?
TUSISEME "gumu jambo", awezalo BINADAMU

IKIWA vyafanywa vyombo, na wenzetu kwa akili,
Vizuri havina kombo, kila jambo kila hali,
VIPI tushindwe kiwambo, hali nasi ngurumbili?
TUSISEME "ni muhali", awezalo BINADAMU.

IKIWA wewe kamili, sawa na wale walivyo,
Binadamu si tumbili, katika hali ilivyo,
VIPI sisi tujidhili, na kujifanya visivyo?
TUSISEME "sisi ovyo", awezalo BINADAMU

IKIWA ndivyo tulivyo, na kama walivyo wale
Bidii iwafunzavyo,ikiwa wasonga mbele
VIPI sisi siwe hivyo, nasi tupande kilele?
TUSISEME “sina ndole”, awezalo BINADAMU.

IKIWA wenzetu vile, kwenye mwezi wamefika,
Hadi wakatua ule, kisa cha kuelimika,
VIPI tushindwe ndwele, magonjwa yakaondoka?
TUSISEME “tuna shaka”, awezalo BINADAMU.

IKIWA ni kutandika, mbingu na yake mawingu,
Nguzo zake kuziweka, hiyo kazi yake Mungu,
VIPI tushindwe kufyeka, mapori tulime Dengu?
TUSISEME “ya uchungu”, awezalo BINADAMU

IKIWA bingwa Wazungu, mambo mengi wataalamu,
Wajua mingi mizungu, ya mengine na elimu,
VIPI sione uchungu, tujifunze kwa muhimu?
TUSISEME “jambo gumu”, awezalo BINADAMU

IKIWA kisa elimu, na maguvu yatumike,
Mbali ya wenda-wazimu, na kazi itimilike,
VIPI isiwe lazimu, nasi pia yatendeke?
TUSISEME "ni upweke". Awezalo BINADAMU

IKIWA siyo wapweke, kumbe sote tu wamoja,
Umbile na fani zake, rangi zetu siyo hoja
VIPI sishinde ufuke, tupate nasi faraja?
TUSISEME "ni viroja", awezalo BINADAMU

IKIWA siyo mauja, hufanyaje na yanoge?
Hata ikawapa tija, ujinga waukanyage,
VIPI sifanye pambaja, na ujinga tuupige?
TUSISEME "sisi bwege", awezalo BINADAMU

IKIWA waunda ndege, vyomo vile vya ajabu!
Wakaranda kama nzige, mawinguni wakaghibu
VIPI nasi tusiige, twondoe yetu taabu?
TUSISEME "tatusibu", awezalo BINADAMU.

ALIKUWA MWANADINI: Licha ya sura hiyo ya kisiasa alikuwa mwanadini na muumini mzuri ambaye hakuwa na ubaguzi wa kidini, ndio maana pamoja na kuwa yeye alikuwa ni Mkristo wa Roman Katoliki, mwaka wa 1966 aliteuliwa kufanya kazi katika mahakama ya Kadhi ya dini ya kiislamu Ilala – Dar –es- Salaam. Alifanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa. Pia rafiki yake nambari moja alikuwa ni Hayati Sheikh Kaluta Amri Abedi ingawa Sheikh Kaluta alikuwa Mwislamu wa dhehebu la Ahmadiyya. Katika uga huo wa dini alitunga vitabu vya tenzi za kidini "*Utenzi wa Injili Takatifu*" NA "*Utenzi wa Zaburi*".

UKUZAJI WA LUGHA YA TAIFA YA KISWAHILI: Alikuwa mstari wa mbele katika ukuzaji wa lugha ya Taifa ya Kiswahili, akiwa na mtaalamu mwingine wa Kiswahili wa kutoka Mombasa Sheikh Shihabuddin Chiraghdin waliandika vitabu juu ya Historia ya Kiswahili. Katika uga huo wa kukuza lugha ya Kiswahili alikuwa miongoni mwa wasisi wa chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA) akiwa pia Rais wa chama hicho.

Natumia fursa hii kuwaomba wadau wengine wa lugha ya Kiswahili kujitokeza na kuchangia gharama za uchapishaji wa vitabu vingine vya Hayati Mathias Mnyampala kama nilivyovielezesha hapo juu.

Basi namshukuru sana Mwenyeezi Mungu kwa kubariki jitihada yangu hii hadi kuwezesha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Charles M. MNYAMPALA (mtoto wa pili wa Hayati Mathias Mnyampala)

S.L.P 2564

Dodoma, TANZANIA

Simu N° : 0755 860581 au 0787 860581 au 0657 373704

Barua-Pepe: charlesmnyampala@yahoo.com

# *MAISHA NI KUGHARIMIA*

## *UTANGULIZI*

Binaadamu hanyamazi hata ukimwona yu kimya lakini moyoni anasema ; na kama akilala usingizini lakini kichwa chasema kwa njozi zake. Basi binadamu moyo unavyompigapiga kama mwendo wa saa ndivyo mawazo yake yanavyokwenda kila wakati mpaka amefikia mauti kusafiri safari kubwa ndipo anaponyamaza. Maana roho inakwenda kwanza maisha mengine mapya huko ahera. Yakiwa mema au mabaya.

Ingawa mimi nilijitia shughuli ya kuandika vitabu vingine vilivyopita, na kushughulikia kuhifadhi habari za kabila langu. Nilishughulika sana kwa kukusanya habari hizo kwa muda usiopungua miaka kumi na moja. Hata mwisho nikafanikiwa kutoa kitabu hicho cha "HISTORIA, MILA NA DESTURI ZA WAGOGO WA TANGANYIKA" kilichotolewa mwaka 1954. Kwa vile mawazo yangu hayakuwa na Nanga ya kuyasimamia mahali pamoja. Kila mara yanatangatanga. Na kutangatanga kwake kumenilazimu mimi kutunga kitabu kingine kinachohusiana na maisha yangu mimi mwenyewe. Maisha ya wafu kuna namna nyingi duniani. Baadhi ya wengine hujaliwa maisha ya utajiri wa mali ; na wengine fahari ; na baadhi yao bidii, na katika bidii hiyo huwafanikisha hata wakafaulu wakawa kama wafu wengine mashuhuri kwa ajili ya akili na bidii zao. Bidii na utendaji pengine huniletea mwenyewe bahati mwishoni[2].

[2] Ukurasa mmoja wa mswada ulioandikwa kwa mkono na Mathias E. Mnyampala unalingana na ukurasa mmoja wa kitabu, maandishi yake yawe marefu au mafupi (mhariri).

Kitabu hiki kinaitwa jina la *"Maisha ni kugharimia"*. Asili ya kupewa jina hili kuna maana kamili. Utastaajabu sana ukisikia kwamba mtungaji wa kitabu hiki hakujaliwa kupelekwa shuleni na wazazi wake mpaka alipokwisha balehe, na baada ya kuozwa na kulipa kodi ya serikali kama vyeti viwili. Ndipo alipoanza kusoma shule za vijijini hata sasa amefaulu kama watu wengine waliopata bahati ya kupelekwa shuleni na wazazi wao au jamaa zao. Hii ndio maana ya jina la kitabu hiki kuitwa *"Maisha ni kugharimia"*.

Duniani kitu bora ni kuwa na moyo mkuu. Watu wengine wengi hukata tamaa na kurudia njiani. Kukata tamaa kunamletea mtu kufifia kwa maisha yake. Jaribu-jaribu mpaka umeona umefaulu kabisa. Ukishindwa usikate tamaa. Duniani hatukukaa kwa raha ni taabu tu. Lazima kushughulika siku zote tu za maisha yetu hapa duniani. Si mfalme, si tajiri, si maskini, si fukarai, siku zote twashughulikia. Wewe ukisema labda mfalme ndiye mwenye raha, la !

Maana halali usingizi upesi akifikiria namna ya kuendesha nchi yake ili ipate kusitawi, au kufikiri namna ya kujiweka tayari iwapo itatokea mashambulio ya ghafla ya adui zake na jinsi gani atende hata ashinde. Kadhalika tajiri nae hufikiri sana jinsi ya kuendeleza utajiri wake, au sivyo atapotewa na utajiri na kumjia umasikini ambao utamletea hali mbaya.

Mawazo hayo huwaletea kukosekana kwa usingizi. Na fukara vile vile namna ya kushughulika ili apate riziki yake. Kwa hivyo ulimwenguni “Maisha ni kugharimia”. Walimwengu husema “Shida ni mwalimu wa maarifa” ni kweli. Tena wanasema : “Ajizi ni nyumba ya njaa”.

Basi usishindwe. Jaribu jaribu tu mpaka uone mwisho wake. Nani ashikae mundu na shoka kufyeka poli hata ashike jembe kulima akakosa mavuno ? Taabu na mashaka ulimwenguni ndivyo tulivyoahidiwa – bidii na jasho letu ndio raha yetu, na Elimu bila jitihada utarudia njiani na kushindwa mitihani. Piga moyo konde kuendelea hata ukiwa mkubwa mpaka umefaulu kabisa, au kadiri yake.

# *SURA YA KWANZA*

## *UTOTO WANGU*

Mimi nilizaliwa katika nchi ya Ihumwa mwaka 1917 yadhaniwa Januari, tarehe haijulikani. Ihumwa ni kijiji cha karibu na mji wa Dodoma. Habari zote za kabila na milango ya wazazi wangu imekwisha elezwa katika kitabu changu cha "*Historia, mila na desturi za Wagogo wa Tanganyika*". Hivi sasa nafuata habari za maisha yangu tu.

Baada ya kuzaliwa mimi, yasemekana kwamba nilitunzwa vizuri sana na wazazi wangu wote. Kwa sababu mimi ni mtoto wa kwanza kwa wazazi wangu. Matunzaji hayo yanasifiwa ingawa sikutunzwa namna ya malezi ya kisasa ambayo ni ya kizungu. Baba alikuwa fundi chuma mhunzi ndiyo kazi yake mwenyewe kwa maisha yote aliyoitumikia na mafanikio ya kazi yake yalileta kwake utajiri wa mifugo si fedha. Mifugo hiyo ni ng'ombe na mbuzi hata mwenyewe niliikuta baada ya kukua.

Kupendwa kwangu na wazazi wangu wote kulithibitika baada ya kupata maizi ya utu uzima. Ingawa nilijua kuwa napendwa, lakini mapendo hayo yaligeuka karaha kwangu kwa sababu nilitambua kama mzee wangu baba alikuwa kama hanipendi.

Karaha hiyo iligeuza imani yangu kwa woga. Mara nyingi nilijifikiria kuwa labda ndiyo utumwa wausemao kwamba "watoto wa watu zamani walikuwa wakiuzwa kwa watu wengine wakawafanya watumwa wao". Kila nilipotaka kukimbilia kwa mama nilijiona kuwa huruma yake haikunitosha.

Vita hivyo vilitulizwa na rafiki mwingine ambaye kwa hakika huko ndiko nilikopata faraja ya kufuta majonzi wangu. Na mtu huyo alikuwa babu na wapili wake bibi. Wote hawa ndio wazazi wa mama yangu. Urafiki huo sikupenda kuucha kwa sababu niliona kwa nafsi yangu kwamba hapana faraja wala huruma na pa kukimbilia kuliko hapo kwao. Ingawa nikipendelea sana kukaa kwa babu mara kwa mara nilifuatwa kuja kuchukuliwa na baba makusudi ya kwenda nyumbani kufunzwa kazi ya kuchunga wanyama. Kazi hiyo ilinichosha sana kwa vile nilikuwa ningali mdogo bado. Kwa hivyo ilikuwa taabu sana. Sababu ya haraka ile baba maana hakuwa na mtoto mwingine wa kuchunga isipokuwa alikuwa akiazima watu wengine ; zaidi wapwa zake, nae aliendelea tu na kazi yake ya uhunzi. Nami mwisho nilizoea nakukulia juani kila mara kuchunga porini.

Japokuwa ni hivyo alinifuata porini ghafla kunikagua kama naangalia mbuzi au hapana. Nakumbuka siku moja aliponikuta nacheza tu na mbuzi wako mbali, loo ! Alinitandika kweli kweli na mijeledi.

Vile vile nakumbuka siku moja Simba alipokamata mbuzi machungani ghafla mimi nilikuwa sijamjua Simba mpaka nilipoambiwa na wenzangu niliokuwa nachunga nao, nikaogopa sana ! Lo mama kusikia hivyo alisikitika sana kuwa “mwanangu atakuja liwa porini”. Lakini vile vile nashukuru sana kwa faraja ya baba ilikuwa baada ya miezi fulani hunichinjia mbuzi mnono kunipa nyama nzuri nzuri na mafuta na mchuzi.

Hiyo ni faraja kuu sana na kutukuzwa sana wakati huo nami nilikuwa nikishawishika sana kwa kushikilia uchungaji wangu. Hata nilipofikisha umri wa miaka saba nikatogwa ndewe na kung'olewa meno mawili chini kama mila inavyotaka. Uchungaji ilikuwa ndiyo kazi yangu maalum kuliko kwenda shamba au popote.

Wakati ule nilikuwa nikisikia kuwa kuna wasomaji wengine huko upande wa kijiji cha Kilwana. Watoto wa hao wasomaji tulikuwa tukikutana nao huko mtoni wakati wa kunywesha wanyama. Lakini nafsi yangu nilikuwa nikifikiri kuwa "wasomaji" ndilo kabila lao, hao hukaa mahali pamoja huko kunakoitwa Missioni. Nilisikia kuwa wana vitabu lakini mimi sikujali vitabu ni nini bali nilijali tu uchungaji wangu na wanyama wangu.

## *SURA YA PILI*

## *KUHAMA NA MATOKEO YAKE*

Baada ya hayo wazee wangu walikusudia kuitoka nchi ya Ihumwa kwenda huko mbali sehemu za magharibi. Uhamaji huo zaidi ulishikiliwa na baba ambaye mjomba wake mwingine alikuwa amehamia huko kitambo na yasemekana kuwa amesitawi vizuri sana. Basi walitengeneza safari yao kamili. Mnamo mwaka 1925 wakaondoka na makundi yao ya wanyama kuelekea Kinyambwa.

Lakini tulipofika Dodoma ya Biringi aliwakuta kaka zake watatu watoto wa baba yake mkubwa walimzuia asiende safari hiyo, kama amechukia kukaa kule Ihumwa afadhali wakae pamoja hapo Dodoma. Tulikaa hapo na kulima hapo katika nchi ya Dodoma. Mimi uchungaji wangu niliendelea nao tu daima. Hapo Dodoma ng'ombe zetu tulikuwa tunanywesha huko katika Bwawa la Muyuji. Watoto wenzangu walianza kunifundisha jinsi ya kuogelea bwawani, hata wakati moja nilikaribia kufa maji nilipofika mahali palipo parefu sana.

Mwaka huo hatukupata amani nyumbani mwetu kuna wakati mmoja nilipokuwa huko machungani nilipanda juu ya mti mkubwa makusudi ya kukata fimbo na mijeledi, mti ule ijapokuwa ni mkubwa wakutosha uling'oka toka shinani na mizizi nikaanguka pamoja nao mpaka chini.

Niliumia lakini si sana. Mbuzi na ng'ombe walikimbia kwa kishindo hicho. Punde si punde mama alikuwa na mtoto wa kike akinyonyesha akafariki dunia ; mama mdogo (mke wa baba, mke wa pili) nae alikuwa na mtoto mwanamume akafariki dunia wakati ule ule. Basi baba hakuona raha akaazimia kutimiza safari yake ya kuendelea mbele huko Kinyambwa, lakini mimi nilirudishwa Ihumwa kwa babu kujitazamia hali ya mwili maana nilikuwa naumwa-umwa, nae mzee akaendelea na safari yake kwenda Ntangano-Kinyambwa. Wakati huo hakuna mtu yeyote aliyethubutu kumzuia tena kuwa asiende, aliendelea akafika.

Japokuwa baba aliendelea na akina mama na ndugu zangu wadogo kwenda huko Kinyambwa lakini huku nyuma Ihumwa kwa babu niliugua sana : karibu kukata roho. Walitafuta waganga wa kienyeji kunitibu haikuwezekana. Hivyo babu alituma habari kwa baba na mama upesi sana. "Uchungu wa mwana aujua mzazi", mara walifika kuniona. Mimi wakati huo sikujitambua ndewe wala sikio ! Ni ajabu wazee wa zamani hawajui matibabu ya kizungu ni nini ; hawajui faida ya Hospitali. Kwa hiyo wazee wangu waliamrisha tu nibebwe na kupelekwa kwenda kuuguzwa huko, na kama kuna hatari ya kufa nikafie huko ugenini. Basi walitengeneza machela na kuchagua watu wengine wanane kunichukua kwa zamu njiani kuachiana, lakini kwa malipo.

Basi waliondoka Ihumwa jogoo ya kwanza usiku. Dodoma mjini walipita alfajiri. Waswahili wa mjini walikuwa wakisema kwa sauti : “Hao wana maiti wanapeleka Hospitali” ; na wengine nao walisema : “Hapana wana mgonjwa wanampeleka Hospitali”. Lakini wapi walipitiliza tu wanakwenda na machela yao hata kumi na mbili labda wakawasili huko Ntangano kwa mtu mmoja aitwae Lugoleyi ambaye ni mjomba wa baba, na ndipo walipohamia.

Baada ya kufika huko wale watu walionichukua wakapewa maksai moja ya ng’ombe (kongolo) wakachinja wakala kuondoa maumivu yao, na wakafunga safari yao kurudi Ihumwa. Mimi kwa hakika sikujijua mwenyewe jinsi gani nilifika ugenini kule, ilikuwa kama njozi tu zilizonifikia usingizini. Kweli ilikuwa bahati mbaya au mwaka mbaya – Kule nilimkuta dada niliyonyonya nikamwachia nae mgonjwa vile vile. Walitafuta waganga wa kienyeji kututibu mimi na dada. Nakumbuka mganga mmoja jina lake Ngalya alitoka Ngalanda katika nchi ya Luatu, huyo hasa ndiye aliyesaidiwa na Mungu akatuponyesha, lakini karibu mwaka mzima. Mwaka huo ndio 1926.

Kwa kuugua sana mimi nilikuwa nashindwa kutembea miguu inachonyota mifupa, lakini mganga huyo ilikuwa kila siku alfajiri nachukuliwa mimi natumbukizwa ndani ya kisima cha maji ya kunywesha ng'ombe yaliyo baridi sana kukaa humo mpaka saa tatu mchana ndipo ninapotolewa, mwisho nikapona kabisa.

Baada ya kupona sawasawa nikarudia tena kazi yangu ya kuchunga, ng'ombe na mbuzi walikuwa wamekwisha zidi sana kwa wingi na kazi ya baba ya uhunzi yaendelea moto mmoja. Wakati huo mimi umri wangu ni miaka kumi hivi.

# *SURA YA TATU*

# *JANDO. MAMBO YA UJANA NA KUOA.*

Hivyo baada ya mimi kupona kabisa na kupata nguvu na afya wazee wangu waliazimia kunipeleka jandoni baada ya mavuno ya kwanza katika nchi ya ugenini tulikohamia. Hivyo babu nae (mzaa mama) alinidai kuwa anatamani kunitia mimi jandoni, na wazee wangu hawakumvunja walimkubalia. Hivyo ndivyo ilipasa tena mimi kurudishwa Ihumwa kwa babu kutahiriwa. Wakati huo mama alikuwa mjamzito. Baada ya kuandaa mambo yote tayari ilipikwa pombe na vitu vingine vinavyohusiana na majando. Nilipelekwa jandoni mimi na wenzangu ambao sitawataja hapa. Siku hiyo niliyoingia jandoni na ndiyo siku mama alijifungua vile vile mtoto mwanamume ambaye ndiye Sosthenes.

Majando yetu yaliendelea vizuri sana kwa furaha zinazohusiana. Ng'ombe saba, kondoo mbili, mbuzi mmoja walichinjwa kwa vipindi mbali mbali nasi katika kikosi chetu tulikuwa wawili tu na ndugu yangu mwingine wa mtoto wa kaka ya baba.

Mwisho mambo yote yakatimia na muda wetu ukawa umekwisha ikafanywa nasi wawili tukatolewa, huu ulikuwa ni mwaka 1927, kama mwezi wa Agosti hivi. Baada ya kutolewa toka jandoni kule Ihumwa mimi nilirejea kule Kinyambwa tulikohamia. Mwaka ule niliumaliza kwa furaha za ujana wangu kwa desturi za mila ya kabila langu, na kuendelea na uchungaji wangu kama zamani.

Niliendelea na hali hiyo hata mwaka 1929 ilitokea shida kubwa sana ya kiu ya maji kwa kunywa watu, zaidi ng’ombe walihangaika sana. Shida hiyo iliishia mwaka 1930 ambapo mvua ilinyesha kubwa sana ambayo iliitwa “Linghumhula” maana yake mvua kuu.

Mapema ya mwaka 1931 niliozwa mke na wazee wangu, kwa mahari ya ng’ombe ishirini na tatu. Mwaka huu nilitokea kuwa maarufu sana katika kijiji changu na majirani kwa ajili ya umaarufu wa ufundi wa ngoma ya kienyeji iitwayo “NINDO” kuwa kiongozi (mwimbizi). Shughuli hiyo ilinifanya niwe maarufu na mpenda ngoma hiyo sana, na kupendwa sana na vijana wa nchi yangu, hasa mzee wangu alifurahi sana kuona sifa yangu ambapo nilitegemewa na wengine. Mwaka huo 1931 niliandikwa kodi ya kichwa. Niliishi na mke wangu salama na kwa upendo hata akavunja ungo, maana nilimwoa kigori.

Katika mwaka 1933 mwezi Agosti nilitamani shule ambapo wakati huo tuliwasiliwa na mwalimu mmoja toka Bihawana misioni kuja fundisha watoto nchini nyumbani kwa mzengatumbi (mkuu wa kijiji). Nilipofika kutaka kuandikwa shule nilikuwa na udongo kichwani mwangu. Mwalimu alikataa kuniandika kwa sababu nilikuwa mlipaji wa kodi, tena nimeoa hilo lilinileta kizuio kwangu.

Japokuwa ni hivyo nami sikukata tamaa, nilihudhuria kila siku kukaa pembeni nikiangalia watoto wanavyosoma, nami nakariri moyoni. Kadiri ya wiki moja hivi mwalimu aliniuliza “mbona wewe unapenda kuja kila siku?” Nami nilimjibu: “Hapana mwalimu, napenda kuja kuangalia watoto wanavyosoma”. Akaniambia: “Hebu jaribu nawe kusoma”. Basi nilisoma yote yaliyokuwemo humo ubaoni. Kufanya hivyo kulimtia moyo wa kuniandika ili niendelee na masomo yangu. Basi niliandikwa.

Maendeleo yangu yalimfurahisha Mwalimu Damiani, tulipofika mwisho wa mwaka ule nilikuwa najisomea vitabu kadha wa kadha, zaidi kitabu cha Esopo na vitabu vya Dini. Nilikuwa nimetamani vikubwa kuendelea na masomo yangu, hasa kwa tamaa ya Dini nilipokuwa nikifunzwa na Mwalimu na kujisomea vitabu. Kumbe ulimbwende wangu wa kwanza sikuutamani tena ingawa nilishawishiwa na vijana wenzangu na wazee wa nchi lakini nilikataa kurudi nyuma bali kuendelea mbele.

# *SURA YA NNE*

# *KAZI YA UALIMU*

Baada ya kubabia kwangu kwa masomo kulinihimiza na kupata tamaa kubwa zaidi ya kuendelea mbele. Basi katika mwaka 1934 baada ya kumaliza kulima mashamba yetu tuliondoka mimi pamoja na kijana mwingine kwenda misioni ya Bahi kupata mafundisho, kwa sababu pale Bihawana ni karibu na nyumbani wenzetu watatushawishi pengine tutaacha maendeleo au shabaha yetu tuliyo nayo.

Safari hii tuliondoka katika mwezi Machi 1934 kwenda Bahi. Tulipokuwa kule na Padri Aloys Gasehys wa R. C. M. Bahi kuwa kundini na wengine. Tulikaa Bahi mafundishoni kama mwezi mmoja tu tuliomba tena ruhusa ya kurudi nyumbani kuaga au kuwaangalia sababu katika safari yetu hatukuaga tulitoroka tu. Hivyo Padri alituruhusu kwa muda wa juma moja tu halafu turudie kule shuleni.

Kwa bahati mbaya tulikuta nyumbani kuna vita ya Nzige waliozaa vimatu wanashambulia mashamba. Mimi ilikuwa lazima nikae nyumbani kwa sababu nina shamba na mke kwa hivyo haingelipasa mimi kuondoka kumwachia kazi mke wangu pekee na ambapo haikosi hata faini ingelinifuata nyuma. Kwa hivyo nilikaa nyumbani kushughulikia mambo ya mashamba.

Baada ya kumaliza mavuno ya 1934 nilijitahidi tena kufuata mafundisho hapo Bihawana mpaka mwaka 1934 ukaisha na tulipoanza mwaka 1935 nilihamia Misioni Bihawana kusoma. Kusoma kwetu sikumbuki kama kulikuwa na madarasa sijui. Kwa tamaa hiyo ya kuendelea na masomo siku moja nilifika hapa Dodoma Kikuyu C. M. S. Central School (sasa ni Alliance Secondary School) niliomba kwa wakuu wa shule hii kama wangenipokea mafundishoni. Majibu niliyopewa pale Misioni Kikuyu ilikuwa hivi: "Ulete Shs 30/= kwa mwaka, ama ng'ombe mmoja ndama ndiyo ada ya shule". Hivyo mimi nilishindwa kwa sababu baba hawezi kukubali kutoa ng'ombe kwa sababu ya masomo ambayo yeye hakupendelea sana na habari hiyo, basi nilirudi nyumbani. Baada ya muda kitambo niliendelea tena na mafunzo yangu kule Bihawana ambayo hayakuwa na ada, ada yetu kufanya kazi tu za mashamba ya misioni, na pale Bihawana nilifaidika sana na mambo ya masomo yangu, hasa kazi ya hesabu na jiografia.

Baada ya kuona kuwa nasongwa sana na watu wa nyumbani hasa wazee kwa ajili ya kuacha uchungaji na mke nyumbani, na mambo ya kodi niliyokuwa sijalipa ya mwaka wa 1935 niliondoka Bihawana kwenda nyumbani.

Nilipofika nyumbani nilikaa siku chache niliondoka tena na mke wangu pamoja kuendelea safari ya Bahi mara ya pili. Hivyo niliondoka na mke wangu tarehe 8 Septemba 1935 mpaka Bahi. Kule Bahi niliwakuta wenzangu wengi, hasa waliokuwa wamefuata mafundisho ya dini na ubatizo. Hivyo na mke wangu tulipokewa kundini mwao. Japokuwa ni hivyo mimi nilikaza nia yangu ya mafunzo yote – ubatizo na shule pamoja. Mke wangu alishindwa nilimrudisha nyumbani kule Kinyambwa na kwa maagizo ya Padri Gasehys aliniagiza nikapate barua ya Padri Yohani wa kule Bihawana kama nilikuwa nimeondoka bila makosa mengine, nami nilifanya hivyo kama alivyoniagiza.

Nilifululiza mafundisho yangu yote mpaka tarehe ya 31 Oktoba 1935 siku ya Alhamisi nilipata ubatizo, na kwa maendeleo yangu mema nikawa nimekubaliwa kwenda shule kubwa R. C. M. Central School Morogoro mnamo mwaka mpya 1936. Kwa bahati mbaya ilipofika siku ya kusafirishwa ilitokea vizuio baina yangu kwa ajili ya mke.

Ingawa mimi nilijitetea mbele ya wakuu, na kuwaambia mke wangu nitakabidhi misioni mabwana walikataa nakusema kuwa “Mbona alikuwa hapa akadai kuondoka? Hatutaki lawama hiyo”. Basi nilishindwa ikawa lazima nibaki wenzangu wakaenda.

Nilirudi kule Bihawana nikazidi kuendelea na mafundisho, baada ya kumaliza mafundisho na ya Kipaimara nikapelekwa sasa kazi ya ualimu kufundisha dini katika vijiji vya nje kama walivyo walimu wengine wa dini.

# *SURA YA TANO*

## *MAENDELEO YA KAZI YA UALIMU*

Ilikuwa tarehe 31 Mei 1936 nilipopata Kipaimara kwa askofu Dismas R. C. M. Bihawana. Baada ya hayo ndipo nilipotumwa katika kazi ya ualimu huko Mzogole katika nchi ile ile ninayokaa mimi. Nilishika shule mbili: nyingine nafundisha asubuhi na nyingine saa nane. Niliendesha kazi hii kwa muda wa mwaka karibu. Malipo ilikuwa shillingi saba unusu kwa mwezi kwa shule zote mbili. Kwa elimu yangu na hali ya wakati ule niliona nina pato. Mke wangu alijifungua mtoto wa kike tarehe 8. 9. 1936.

Ingawa nilikuwa mwalimu kwa kweli sikuwa na utalaam wo wote juu ya kazi yangu vema bali niliendelea kufundisha na huku najisomea nakuwaendea walimu wakubwa wenye vyeti vya ualimu hasa kunifundisha. Bidii na bahati ilinifanya niendelee vema kujiongezea maarifa. Nilipenda sana dini yangu.

Hivyo mnamo tarehe 20 Desemba 1936 zilitangazwa nafasi za ukarani huko Bomani Dodoma. Wenzangu walinishawishi kwamba ningejaribu kuuliza nafasi hiyo ningeweza kupata kazi. Lakini mimi nilijidharau zaidi kuwa kazi za kikarani ndizo ngumu sana ambazo huhitaji elimu na maarifa mengi zaidi kuliko kazi za ualimu nilivyofikiria. Kwa kutiwa moyo hivyo niliandika barua yangu ya kuomba kazi Bomani tarehe 29 Desemba 1936. Barua yangu hiyo ilipokelewa na Bwana H. R. H. Butterfield, Bwana Shauri mdogo ambaye aliniambia kuwa ningefika kesho asubuhi, kwa sababu wakati huo ilikuwa ni jioni.

Asubuhi yake nilifika. Kabla ya kuonana na Bwana Shauri niliambiwa na tarishi mmoja aliitwa jina Sasamara alinikemea na kuniambia kwamba maneno yale niliyoandika katika barua yangu ya kuomba kazi hayakuwa mema hata kidogo, hata Bwana Shauri mkubwa amekasirika nayo. Hivyo nilikata tamaa nilianza kutoka nje niende zangu ili kuepuka magombezo ya Bwana mkubwa.

Nilipotaka kutoka mkuu wa matarishi wale jina Mganga Makasi aliniita na kuniuliza nilichofuata hapo Bomani. Nami nilimwelezea nae. Aliingia ndani kuonana na Bwana Shauri mkubwa amwulize habari zangu. Bwana aliniita nikapewa karatasi na kalamu niandike pamoja na hesabu. Nilifanya hivyo tukaridhiana na Bwana Baker Bwana Shauri mkubwa bali nilipewa neno moja la kuchagua kuwa ninapenda kufanya kazi mwezi wa kwanza bila mshahara? Nami nilikubali nikapelekwa kufunzwa kazi huko Dodoma Native Treasury (Hazina ya wenyeji) ya ukarani wa Baraza. Hivyo nilianza tangu 1. 1. 37. Niliendelea na mafundisho hayo hata nilipoelewa vema ikawa niende kufanya kazi ya usaidizi wa karani wa Baraza Kinyambwa ambako ndilo Baraza langu.

Mnamo mwezi wa Julai 37 nilirudi nyumbani nakuacha kabisa kazi hiyo ya usaidizi wa Karani wa Baraza nilijiuzulu mwenyewe. Sababu yake niliugua sana ugonjwa wa macho karibu kupofuka macho yangu.

Baada ya kuacha kazi hiyo na kupona ugonjwa wa macho, Mabwana wa Misioni walinidai tena kurudi katika kazi yangu ya ualimu na kwamba maongezo ya mshahara wangu yatakuwapo. Hivyo nilishika kazi yangu katika vijiji viwili: Mpinga na Nthangano kila shule shillingi saba unusu (Shs 7/50 X 2) = Shs 15/=. Nilifanya kazi hiyo kwa maendeleo mema mpaka mwezi Desemba tarehe 15, 1937. Nilitakiwa tena na Mtawala wa nchi yangu kwa vile Karani wake alikuwa amekosa na kuachishwa kazi. Kwa hiyo nilirudi tena kazini kuanzia tarehe 23 Desemba 1937 kuwa Karani wa Baraza la Kinyambwa. Mshahara wangu wa kwanza nilipokea Shs 12/50 nusu ya mshahara wa mwezi ambao ni Shs 25/= kila mwezi.

## *SURA YA SITA*

## *MAENDELEO YA KAZI YA UKARANI*

Baada ya kuanza kazi yangu hiyo chini ya Mtemi Makasi wa Kinyambwa, niliendelea vizuri sana na kazi yangu na kwa mawasiliano kamili na mtawala wangu. Japokuwa niliitwa Karani lakini elimu yangu haikuwa kamili kweli kama walivyo makarani wa leo jinsi wanavyopaswa kushika kazi hiyo kwa uwezo wa elimu zao kamili.

Japokuwa sikuwa na elimu kamili lakini nilijitahidi sana kwa kutaka mafunzo zaidi ya maarifa ya kikarani kwa wenye kujua zaidi yangu. Bidii yangu ilikutana na bahati ya maendeleo mema kwa majaliwa ya Mungu. Watu wa kijiji changu katika nchi yangu walikuwa na mashaka nami sana wakidhani kuwa sitakuwa na maendeleo bali najitafutia kufungwa. Ijapokuwa mashaka walikuwa nayo, nami niliendelea tu kidogo kidogo, kama wasemavyo: "kulega lega si kuanguka".

Mnamo mwaka 1941 nilipata bahati ya kupata sifa njema sana kwa kazi yangu, hasa ya kutoza kodi, toka kwa mabwana shauri wa Boma. Sifa hiyo ililetwa kwa vile kumaliza kodi nchini mapema tangu 1940 na 1941. Kwa ajili hiyo nami nilijulikana na wengine kwa kuwa Bwana D. C. Mr. A. H. Le Geyt alikuwa akitangaza jina langu katika mabaraza mengine ambapo akikuta kodi bado, kama sehemu nyingine ya Dodoma; Mpwapwa na Manyoni (zilipokuwa bado Mpwapwa na Manyoni chini ya Dodoma).

Mwaka huo ulinijia na bahati mbaya vile vile mimi na Mtemi Makasi kiongozi wangu kwa ubovu wa afya. Tangu June nilipata homa kali sana nikaletwa Hospitali Dodoma. Baada ya kupona kurudi tena Mtemi Makasi akawa mgonjwa sana akapata matibabu akapona. Katika mwezi wa Agosti tena nilirudiwa na homa vibaya nikaletwa Hospital Dodoma. Kazi yangu nilishikiwa na kijana mmoja ambaye alikuwa Karani wa kodi kwa Boma. Baada ya kupona mabwana walifikiria hali yangu labda hewa imebadilika vingine wakanipa (Transfer) uhamisho kwenda nchi nyingine ya Hombolo kwa Mtemi Mwaluko. Uhamisho wangu ulitokea mwanzoni mwa mwezi Septemba, 1941.

Wakati huo nilionekana kama Karani hodari kwa kazi zote za kikarani na utaratibu wake. Mabwana wa serikali walitokea kunipenda kwa bahati. Bwana D. C. alinishawishi kama napenda kupata maongezo ya mshahara nibadilishwe toka katika N. A. mamlaka ya wenyeji nifanywe Karani wa kodi wa Boma (Tax Clerk, Provincial Administration) nami nilikubali ikawa mambo yamengojea mwanzoni au mwisho wa mwaka 1941. Katika mwezi Novemba 1941 Mtemi Makasi wa Kinyambwa homa kali sana ilimrudia iliyonitoa mimi Kinyambwa. Ugonjwa huo ulikuwa ndio wa mwisho uliomletea mauti mapema mno tarehe 27. 11. 41. Nilihudhuria katika kilio cha huyu mpenzi wangu na mtawala wangu.

Ahadi ya Bwana D. C. ilitimia kweli mnamo tarehe 24th December, 1941 nikabadilishwa toka katika Native Authority nikawa Tax Clerk katika serikali kuu kwa mshahara wa Shs 40/= kila mwezi, ikawa nimeacha utawala wa wenyeji na mshahara wa Shs 25/= kwa mwezi tokea tarehe 23. 12. 37 ikawa ndio mwisho.

## *SURA YA SABA*

## *KARANI WA KODI NA MAENDELEO MENGINE*

Tarehe 1 Januari, 1942 nilihamishwa toka Hombolo nilikokuwa Karani wa Baraza, nilihamishiwa Makutupora kwa Mtemi Chitindi. Wakati huo nilishika vitabu vya nchi mbili. Baraza la Makutupora na Baraza la Dodoma kwa Mtemi Biringi kutoza kodi, lakini stesheni yangu ikawa Makutupora. Maendeleo yangu kwa kazi ya kodi yalikuwa mema sana na yenye sifa bora.

Wakati huo nikawa na sifa nyingine vile vile ya uandikaji wa Gazeti la *Mambo Leo,* kama habari za miji na maongezi. Uandikaji huo nilianzia Kinyambwa mnamo mwaka 1938 nilikojifunzia, kwa tamaa ya maendeleo nilianza kujifunza kusoma Kiingereza. Nilinunua vitabu vya Kiingereza: kama *Mwalimu wa Kiingereza* na vingine vya masomo ya kwanza kwa Kiingereza. Niliwaghasi sana waliosoma Kiingereza shuleni ili wanifunze, nilikubali kutoa gharama kwao kwa msaada huo na baraka zake Mungu nilianza kutambua kitu gani ninachosoma na ninachofunzwa.

Tamaa ya moyo wa binadamu haina mpaka, wengi wao waliokuwa wakinifunza Kiingereza walikuwa Islamu na wengine Wakristo. Wale waliokuwa Islam waliosoma Kurani niliwaomba wanifunze kusoma Kurani. Waliniandikia katika A. B. C. D. pande mbili Kizungu na Kiarabu. Kwa bahati nilijua kusoma na kuandika Kurani ingawa si kama wao. Naweza kusoma barua na kuandika majibu bila taabu katika lugha ya Kiswahili kwa Kurani.

Taabu nyingi zilinipita kwa kazi ya kodi, maana sikuwa na nafasi kwa kukaa. Ilikuwa safari kila mara bila kupumzika. Ijapokuwa sikuwa na nafasi ya kustarehe lakini jina langu lilikuja na sifa sana. Nilipelekwa kila mahali ambapo kodi ilipoonekana imechelewa kwisha. Bwana D. C. mpya Bwana R. W. Varian alinituma kuingia usandawa wa Wilaya ya Kondoa kwa ajili ya kufuata wananchi waliokimbia kodi toka sehemu ya Wilaya ya Dodoma. Hivyo nilifika kwa Jumbe Athman Haleki wa Farkwa tukawa nae kwa mwanangwa Msangazi Komasi.

Mwezi Oktoba, 1942 nilitumwa kwenda matumbulu kwa Mtemi Huwao; Novemba na Desemba, 1942 nikawa Buigiri na Msanga. Kabla ya kumaliza Desemba 1942 niliitwa na Bwana D. C. kwa simu kuwa niwe tayari kwenda wasilisha fedha ya kodi na Bwana Shauri wa Manyoni ananingoja hapo Bomani kwa safari ya kwenda nae Manyoni.

Mnamo tarehe 15 Desemba, 1942 nilifika Bomani kuwasilisha fedha zao mimi nilisafiri pamoja na Bwana Shauri wa Manyoni H. H. McLery akaniacha katika nchi ya Unyangwira ambapo nilifanya kazi hapo mpaka mwisho wa mwezi Desemba, 1942. Hapa Unyangwira ilikuwa ni safari ya pili kuja maana nilikuwa nimekwisha fanya kazi ya kusaidia kodi wakati nilipofika Desemba, 1940 mara ya kwanza.

Ijapokuwa huu ulikuwa ni muda mfupi tu lakini kazi yote ilikwenda vema sana. Nilirudi Dodoma mnamo tarehe 27 Desemba 1942 kuwasilisha fedha.

Tarehe 1. 1. 43 nilirudishwa tena kule Unyangwira. Kwa sababu Bwana H. H. McLery Bwana Shauri wa Manyoni alinidai tena kurudia huko Unyangwira kuhesabu watu wote walipaji kodi na kuandika kitabu kipya cha kodi. Hesabu ya Unyangwira ilikuwa imeharibika kwa sababu walipaji kodi wengi walikuwa wamekwenda vitani kazi ya askari K. A. R. na wengine huko Muheza kwa kazi ya kugonga mpira, na kwa taabu iliyotokea ya ugonjwa wa shingo wengi walikufa na wengine walihama. Basi niliandika na kuhakikisha hesabu kamili ya waliopo nikaandika vitabu vinne nikamaliza, baada ya kumaliza nikarudi Dodoma.

Dodoma sikukaa sana nilitakiwa tena niende huko Mgunduko. Katika Baraza la Mgunduko nilifika mwezi Machi 1943 nilianza kuandika hata niliombwa nizipitie nchi za juu zilizo ndogo kama Nkonko na Mdaburo, kazi hii nilikuwa nimeizoea sikukawia nilimaliza mwishoni mwa mwezi, nikarudi Dodoma. Baada ya kufika Dodoma nilitakiwa tena niende Manyoni, nilikwenda. Bwana H. H. MacLery alinituma tena kwenda katika Baraza la Itigi kuandika.

Huko Itigi nilifika tarehe 4 Aprili, 1943, nilifanya kazi mwezi mmoja nikarudi Manyoni Bomani, na Bwana Shauri akaniruhusu hivyo kurudi Dodoma kabisa.

Dodoma nilifika mwanzoni mwa mwezi Mei, 1943, kuonana na Bwana R. W. Varian akaniambia kuwa tuende nae kwenye minada ya ng'ombe, kwa amri iliyotolewa ya kupunguza wanyama kwa kuwauza ng'ombe na kupelekwa vitani kwa askari. Tuliondoka nae katika minada hata kufika Kigwe nilitumwa tena na Bwana nifike Kinyambwa kuangalia wakili Mnapa wa huko anafanya nini mbona haleti watu wa kwenda Muheza kwenye kazi ya mpira? Nilifika huko na nilirudi na watu pamoja nilimkuta pale pale Kigwe mnadani. Lakini nilimwambia kuwa naumwa sana akaniruhusu kurudi Bomani, lakini hasa moyo wake haukupendezewa.

Aliporudi safari alinituma tena kwenda Zanka kwa Mtemi Chonya kutoza kodi. Niliendelea na kazi huko tangu Juni mpaka Agosti 1943 ndipo nilipopata kuambiwa na D. C. wangu kuwa Bwana Shauri wa Manyoni ananidai, kwamba kuna mgogoro wa majumbe wanagombania mpaka, niende nikawaamue nikakate mpaka mpya kwa idhini yake.

Hivyo nilisafiri Manyoni. Sikumkuta Bwana H. H. MacLery alikuwa amekwenda Mpwapwa amekuja mgeni J. S. E. Griffiths akanipokea. Nilikwenda kukata mpaka wa Makutupora na Kisongo kwa majumbe Shomi na Mtandi nikamaliza. Nilipotakiwa kurudi Dodoma kwa vile sifa ilikuwa njema Bwana huyu mgeni alinizuia nikakaa Manyoni kabisa kuwa ni uhamisho wangu kutoka Dodoma.

## *SURA YA NANE*

## *MAENDELEO YA KAZI MANYONI NA MWISHO WA KAZI YANGU. NA MENGINEYO.*

Nilikaa Manyoni tokea Septemba, 1943 katika Baraza la Unyangwira kwa Mtemi Mombo. Mnamo mwezi Januari, 1944 nilipelekwa Mdaburo, Nkonko na Isseke kwenda kuandika hesabu ya walipa kodi huko maana hesabu yao ilikuwa imepungwa sana. Kazi hiyo ilimalizika mwishoni mwa Januari nikaenda Manyoni Bomani. Mwezi Februari, 1944 nikapata uhamisho kwenda Itigi kutoza kodi ya madreva wa watumishi wengine wa Railway. Eti ilisemekana kuwa walikuwa wakaidi zaidi kulipa mbele ya Karani wa Mtemi Andu.

Nilikaa Itigi nikashika madaraka hayo kama nilivyoagizwa, ikawa nimeongezewa mabaraza mengine matatu zaidi. Nayo ni Kirurumo, Jiwe la Singa na Itumba kuhimiza kodi na kusaidia kazi nyingine nyingi zilizohusiana na mambo ya Serikali. Baada ya hayo nikaandika Daftari zingine mpya za walipaji kodi. Nilikaa Itigi, Kirurumo, Jiwe la Singa na Itumba mpaka mwisho wa mwaka. Kwa bahati mbaya mnamo mwezi Novemba, 1944 Mtemi Kilomo wa Baraza la Itumba aliachishwa Utemi. Bwana D. C. na Bwana Shauri Bwana P. Gawthorne walitaka mimi nishike kazi ya uwakili kuongoza Baraza hilo mpaka amepatikana Mtemi. Lakini mimi nilikataa kabisa. Ndipo nilipolazimishwa na Bwana Shauri nitafute mtu mwingine akachaguliwa mkuu wa kijiji Katembo kuwa Wakili wa nchi ya Itumba.

Tarehe 20. 12. 44 nilipata livu kubwa nikarudi kwetu Dodoma mpaka tarehe 14. 2. 45 nikarudi kazini huko Manyoni. Nilipofika tu Manyoni ndipo ilipoanza kazi ya uandikaji au kuhesabu wanyama – hasa ng'ombe kwa ajili ya kodi ya ng'ombe ilipoanza. Nilitumwa kuhesabu ng'ombe na walipaji kodi katika nchi ya Muhalala kwa Mtemi Paulo Messomapia. Huo ulikuwa mwezi Machi 1945, nilimaliza kazi zote, na Aprili 1945 nikaenda nchi ya Mgunduko, nilimaliza na mwezi Mei 1945 nikawa Unyangwira tulikuwa wawili tukamaliza.

Wakati huo Bwana J. E. S. Griffiths alikuwa amepata uhamisho kuja Dodoma na sisi kule Manyoni tuliangaliwa na Bwana C. C. Harris Bwana Shauri. Bwana huyu ndiye aliyeanzisha kazi ya kodi ya ng'ombe. Ingawa nilikuwa na bahati ya kupatana na mabwana wengine huyu haukuwa upepo wangu hasa kwa kazi yake ya uandikaji wa ng'ombe, na mengineyo ya chuki kwangu. Kazi ya uandikaji vitabu vya kodi ya watu na ng'ombe iliishia mnamo mwezi Juni, 1945. Baada ya kuona vitabu nimeandika tayari nikapewa barua ya kuacha kazi eti kwa sababu ya kupunguzwa makarani. Nilicha wakati huo mshahara wa Shs 46/= kwa mwezi.

Basi nilikaa kungojea mwezi wangu uishe nirudi kwetu Dodoma. Tarehe 31. 7. 1945 nikaacha kazi nikapata nauli yangu. Siku hiyo ilikuwa Jumanne nilipanda gari la abiria nikarudi Dodoma pamoja na barua ya Bwana Shauri kumletea D. C. ili nipate Hati yangu ya kazi (Certificate of Service). Na Jumaatano 1. 8. 1945 nikapewa Certificate yangu mikononi mwa Bwana J. E. S. Griffiths. Certificate hiyo iliandikwa hivi[3]:-



TANGANYIKA TERRITORY

Local
[redacted] Civil Service—CERTIFICATE OF SERVICE

Name of Officer Mathias Mnyampara

Position held and Department: Tax Clerk, Provincial Administration.

Period of service: From 1/1/1942 to 31/7/1945.

Cause of termination of engagement: Retrenchment.

Efficiency: Fair.   Dod/5/140 3-10-56

General conduct: Good.

J.E.S.GRIFFITHS, D.C.
*Head of Department*

Date 1st August, 19 45.

Right thumbprint of bearer, or signature

Efficiency and General Conduct are assessed as "Very Good," "Good," "Fair" or "Indifferent."

G P Dsm 47312/12-41/2m

x Previously worked for Native Authority as from 23/12/37 to 31/12/41.

CERTIFIED TRUE COPY.

27th February, 1947.

DISTRICT COMMISSIONER, DODOMA.

© ROY 2007 (picha)

[3] Kinanukuliwa kwa mkono katika mswada. Nitanukulu vyeti vyenyewe vikiwa vinapatikana (mhariri).

Basi nilipopata cheti changu nikarudi nyumbani kukaa nikapata nafasi ya kufungua kazi zangu za mashamba, na nikapata nafasi zaidi ya kujiendeleza na masomo yangu ya elimu ya ukarani hasa Kiingereza.

Baada ya kulima mwaka 1946 Januari nilipeleka barua yangu kwa Bwana mkubwa wa kazi ya Ndorobo Shinyanga. Majibu yalikuja mema waliomba vyeti vyangu cha shule na vya kazi. Nilipeleka cheti changu cha kazi, na cha shule niliwaambia kuwa sina, sikupata cheti cha shule. Nililetewa majibu ya kuniita pamoja na "Government Warrant" ya nauli ya kuendea. Ijapokuwa niliandika barua yangu kwa lugha ya Kiingereza kibovu nilikubaliwa nikaenda Shinyanga. Kazi niliyotakiwa ilikuwa: "African Assistant, Entomologist Laboratory". Dodoma niliondoka Februari 10, 1946 nilifika Shinyanga 11 Februari alfajiri. Nilipokewa na mabwana wengine mjini nilishinda hapo. Mnamo saa 10 mchana nilipata motokaa ya Bwana mkubwa wa huko, kwa jina aliitwa Captain Findler alinipeleka mpaka huko Shinyanga ya zamani kwa Director of Tsetse Research Department.

Wakati huo tulikuwa wawili na mwingine mwenzangu aliyekuja toka Morogoro. Hivyo tulikabidhiwa kwa Afisa wa kazi yetu Bwana Whatsite. Tulizungumza nae hata akatupatia mahali pa kufikia, na asubuhi tulikwenda offisini tukagawiwa kazi zetu. Mshahara wetu ukawa Shs 50/= kwa mwezi.

Lakini mimi sikustahamili sana maana baada ya mafunzo ya pale offisini lazima kwenda porini kuchukua mafunzo ya kukamata Ndorobo ujue jinsi ya kuwanasa na kuwatambua vizuri madume na majike na damu waliyo nayo ni ya mnyama gani? Au ya binadamu utambue kabla ya kwenda kuipima na darubini. Mimi nilishindwa kwa hofu ya simba na majoka porini baada ya miezi michache niliomba kubadilishwa, nao wakakataa nikaacha kazi nikapata mshahara wangu nikapewa nauli nikarudi nyumbani Dodoma.

## *SURA YA TISA*

## *MAKAO YA NYUMBANI – KAZI YA STOO NA NDOROBO.*

Baada ya kuacha kazi ya Ndorobo kule Shinyanga nilirudi Dodoma. Katika tarehe 25 Agosti, 1946 nilianza kazi ya Stoo ya njaa kule Manyoni chini ya A. G. Stephen D. O. wa Manyoni. Kazi hii ilikuwa na taabu na usumbufu na huzuni nyingi sana. Kila mara tulizika watu waliokufa na njaa ya "LIHAMBAYA" kwa hiyo tulileteWa sururu na vyombo vingine kama mitalimbo kuchimbia Makaburi kuwa tayari kuwazika wanokufa kwa njaa. Kwa kazi hii ya Stoo sikuwa na furaha kamili, maana kama mjuavyo mwenye pato ndiye kuandamwa siku zote. Fitina ilikuwa nyingi sana, kuwa natumia cha Serikali kilichotolewa kwa wenye njaa kwa njia nyingine. Hivyo ilikuwa mara kwa mara mabwana huja ghafla kutaka kuangalia hesabu yangu na kukagua baki ya magunia yaliyomo ndani ya Stoo, lakini walikuta hesabu yangu inalingana ndani ya vitabu na baki ya magunia. Mwenendo huo na upelelezi mwingi ulipopita ilionekana ni fitina wazi, wakaniacha niendeshe kazi yangu, na wafitini wakafa moyo.

Stoo ya njaa Manyoni ilifungwa mnamo 30 Aprili, 1947 watu wamekwisha pona njaa. Kwa bahati mwaka huo nami nilikuwa nimelima shamba katika fyeka ya Ndorobo Muhalala nilifanikiwa sana kwa mavuno, kwa hiyo nilipendelea kukaa pale kuangalia shamba langu na mavuno mpaka nivune. Ijapokuwa nilikuwa na nia ya kuangalia shamba langu la Eka kumi lakini Bwana Ndorobo aliyekuwa akifyekesha pale Muhalala alionana na Bwana Shauri baada ya kazi yangu kufungwa ya Stoo kuwa angependa kama Bwana A. G. Stephen ataniruhusu kuwa nae kwa kazi ya Ndorobo kule Makasuku Tsetse Clearing Camp.

Bwana Shauri alimkubalia, wakatuma matarishi wawili kuja kuniita na kuwasilisha hesabu yote ya Stoo magunia yaliyobaki. Hivyo nilikwenda kuwapa hesabu yao magunia yaliyobaki hayakuwa mengi sana yalikuwa magunia themanini na mawili na nusu (82½). Hesabu hiyo ndiyo iliyokubaliana na vitabu vyangu na baki katika Stoo.

Hivyo tarehe 1. 5. 47 asubuhi nilianza kazi ya Karani wa Ndorobo kule Makasuku. Nilimkuta Karani wa huyu Bwana Ndorobo amepewa barua ya kuacha kazi kwa kuwa hafai kazini. Tulikaa pamoja na Karani huyo kama zaidi ya Juma moja akaacha nami nikaendelea na kazi hiyo kwa bidii kubwa. Affisa wangu huyu alikuwa mkali sana, lakini nashukuru kwa kuwa hakunivunja kauli yangu kila niliposema lenye maana mbele yake.

Fyeka hii ilikuwa kama vita kwa wingi wa watu walioletwa. Manyoni ilileta wafyekaji 1050 na Dodoma 1390 jumla watu 2440. Mimi nilishika Muster Roll na vipande vyao. Kila nilipomaliza kuingiza siku zao na kujumlisha ilinipasa kuondoka kwenda porini kukagua kama wote wapo ama wametoroka na kujificha. Hivyo niliita majina kwa vipande vyao, na wote walitokea kuitika na kupewa vipande kule kule kazini. Vipande ambavyo sikuwapata nilirudi navyo kambini na walipofika kuvitaka iliwabidi waeleze walikokuwa wale walioonekana kuwa hawakuwa na ushahidi wa kutosha walikatwa siku zao.

Wingi wa watu hawa uliwafanya wapate Posho ya kutosha. Walipata unga kila siku, maharagwe chumvi, mafuta ya karanga Sukari Guru na Nyama kila Juma mara mbili. Walichinjwa ng'ombe kadiri ya kutosha watu waliohudhuria kazini siku ile. Kazi zote hizi ziliangaliwa na mimi ingawa alikuwako mwangalizi wa Stoo.

Katikati ya mwezi wa Julai, 1947 Offisa wangu alishikwa na homa kali ikamlazimu apelekwa Dodoma au Dar es Salaam, kwa kutibiwa. Hivyo ilinipasa kushika madaraka yote juu ya Camp ya Ndorobo badala yake. Ilinipasa kuwa macho siku zote. Uangalizi wa Lori la Ndorobo na Dreva wake, wafanya kazi wote na wachunga ng'ombe za Ndorobo na hesabu ya ng'ombe zao. Mara kwa mara alinifikia Bwana A. G. Stephen kunikagua na pengine kunitumia ng'ombe wengine walionunuliwa kwa ajili ya Ndorobo.

Wakati huu kazi hizi nilikuwa nimezizoea bila taabu. Muster Roll Daily Works Allocation, Kuandika Voucher za waliofunga na kulipwa mshahara. Bwana wa kazi yangu aliporudi toka Hospital mnamo Agosti, 1947 alikuta kazi zote zinaendelea moto moja, kwa hiyo alishukuru sana.

Wakati huo tukawa tumepokea Bwana Ndorobo mwingine mgeni toka Arusha ambaye alianzisha fyeka yake huko Itetema akagawiwa wafanya kazi toka hapa akachukua robo ya vibarua waliokuwa hapo Makasuku. Tulipokea barua toka kwa Bwana Shauri Manyoni kusema : "Bwana D. A. Pienaar Tafadhali mruhusu Bwana Mathias E. Mnyampala aende pamoja na Bwana Ndorobo mgeni Bwana D. A. Pretorius huko Itetema amwonyeshe jinsi ya mpango wa kazi hiyo kwa kuwa yeye ni mgeni. Akisha mwongoza na kumtafutia Karani tayari atarudi kwako. Sasa tafuta mwingine wa kukusaidia."

Mimi nilikwenda na Bwana Pretorius mpaka Itetema nilianzisha kazi ya Ndorobo na kuongoza kama ninavyojua hata nilipata Karani mmoja nikamwandika nikamwonyesha namna ya kazi hiyo nikamwachia nikarudi tena Makasuku kuendelea na kazi yangu kama Kawaida. Bwana Pienaar (Tsetse Clearing Officer) alifurahi sana kunipokea tena, nami nilifurahi vile vile.

Baada ya masiku nilizidi kusikia mvumo wa kazi ya Company mpya huko Kongwa. Nilipeleka barua yangu ya maombi ya kazi na nilitaja kazi ninazozifanya hapo Makasuku. Barua hii niliandika kwa Kiingereza, na wakati wote huu nilitumia kuandika barua zangu kwa Kiingereza tu ingawa kilikuwa si kizuri. Nilipokea majibu toka Kongwa kunitaka niende huko kwa mshahara mwema zaidi na huu nilio nao na kazi ni hii hii tu ya Time-keeper overseer. Barua yao ilinifurahisha mno. Sikujizuia nilipeleka barua Bomani ya kuacha kazi. Sikupata majibu mpaka yeye Bwana A. G. Stephen alipofika kuonana nami kuuliza sababu, nami nilimjulisha sababu ya mshahara kidogo. Na Bwana huyu Pienaar alikwisha ng'amua kuwa nakwenda Kongwa alimwambia. Hivyo niliongezwa mshahara toka katika mshahara wa Shs 35/= nikapewa 15/= zikawa 50/=.

Bwana A. G. Stephen alikwenda Livu mnamo Septemba, 1947 nyuma alikuja Mr. R. W. Smith ambaye kumbe alipewa historia yangu na Bwana Stephen, basi alifika Ndorobo akaniita akanambia: "Nasikia unataka kutoka hapa". Nami nilimwambia: "ndiyo". Mwishoni mwa mwezi Septemba nilionana na Bwana Smith kwamba nataka kwenda Kongwa. Nae alinishauri kuwa: "usipofanya haraka nitakusaidia, lakini tutafutie Karani mwingine alie bora nawe utakwenda". Nami nilimwagiza mdogo wangu Andrea Mnyampala toka nyumbani nikamfundisha kazi akaelewa nikawakabidhi.

Kumbe msaada aliosema Bwana Smith ulikuwa: aliandika barua kule Kongwa na Dodoma Labour Exchange ili waweke nafasi yangu mpaka nifike mwishoni mwa mwezi Oktoba, 1947. Karibu ya mwisho wa mwezi wa Oktoba Bwana R. W. Smith alifika kule Ndorobo pamoja na Bwana D. C. Bwana W. A. Forbes wa Dodoma akaniambia nimekubaliwa kuwa nafasi yangu nimewekewa mpaka tarehe 31 Desemba, 1947. Nami nilifurahi.

Kabla ya 31. 10. 47 Bwana Stephen alirudi toka leave. Aliposikia hivi alisikitika sana lakini haikuwezekana kwa sababu ahadi zimekwisha wekwa. Mnamo tarehe 31. 10. 47 nilifika mbele ya Bwana A. G. Stephen kwa safari ya Kongwa, nae aliniuliza kuwa: "Je kama ungestahamili hapa?" Nami nilisema: "Nakubali, lakini je kama kazi itafungwa nyakati za kilimo mnavyosema". Hayo yalimvunja nguvu. Basi akanitengenezea safari yangu "Warrant" mimi na mke wangu mpaka Dodoma, kile chakula nilicholima pale Muhalala niliuliza, Bwana Stephen alinipa "CERTIFICATE OF SERVICE" iliyoandikwa na yeye mwenyewe kwa hati ya mkono wake kwa wino. Bwana A. G. Stephen alikuwa amekwisha nishuhudia vizuri sana tangu aliponiandika kuwa Karani wa Stoo ya njaa, hata aliponibadilisha kuwa Karani wa Ndorobo kule Makasuku chini ya Bwana D. A. Pienaar, na sifa gani alisikia toka kwa Bwana huyu. Kwa hiyo hakuwa na wasi wasi wowote kwa maneno aliyoyaandika katika cheti changu. Kwa hiyo Bwana Stephen aliniandikia hivi:-



TANGANYIKA TERRITORY.

~~African~~ Local Civil Service.

DOD/5/140
3-10-56

CERTIFICATE OF SERVICE.

Name of Officer ....MATHIAS s/o MNYAMPALA....

Position held ) ....(1) FAMINE STORE CLERK N.T.

and Department) ....(2) CLERK TSETSE CAMP N.T.

Period of Service. From (1) 25.8.46 – 30.4.47
(2) 1.5.47 – 31.10.47

Cause of Termination ) .... Tsetse camp closed down during

of engagement ) .... the planting season

Efficiency ....Very Good .... Educated intelligent

.... can use initiative.

General conduct .... Excellent

....................

....................

[signature] ADO/c

DISTRICT OFFICE
Date 31.10.47

.................... Head of Department.

Date ....31.10.1947.

LABOUR EXCHANGE
KILOSA
KLE/5/147
15-6-54

Mathias Mnyampala
Right thumb print of
bearer.

Efficiency and General Conduct are assessed as "Very Good," Good," " Fair," or " Indifferent."

© ROY 2007 (picha)

Nilipopata cheti changu nilisafiri mpaka Dodoma Labour Exchange. Nilipofika Dodoma kabla ya kuonana na Clerk i/c wa Labour Exchange tulionana na Bwana R. W. Smith ambaye alijaribu kunishawishi nibaki pale Dodoma atanipa kazi, lakini nilipoona kuwa mambo yenyewe yana mafikirio nae vile vile aliniambia: "Sitakuzuia zaidi, bora ufike Kongwa. Baada ya miezi miwili au mitatu nitakuletea barua kuuliza kama utakuwa bado unapenda kuishi Kongwa. Lakini ninavyojua Kongwa ilivyo na vumbi lake labda hutapenda kuendelea zaidi". Hivyo nilisafiri Kongwa na nilifika tarehe 4. 11. 47.

## *SURA YA KUMI*

## *KARANI KATIKA PAULING & CO. LTD KONGWA NA MAREJEO KATIKA BOMA DODOMA.*

Mnamo tarehe 5. 11. 47 ndipo siku tulipopelekwa kupimwa na Bwana Mganga. Tulihudhuria saa nane pamoja wengine. Kwa bahati nilisifiwa kwa afya yangu. Baada ya hayo nikawa nimeandikwa. Nilikuwa katika namba 240 ya makarani ndani ya kitabu. Labour Officer Bwana Bobet alinipeleka kwa Chief Time-keeper, Bwana Paterson. Nilipokewa nae na kuniuliza maswali machache kwa Kiingereza akaniandikia barua kupeleka kwa Chief Cashier, Pauling & Co. Ltd. Bwana huyo alinikaribisha vizuri na nikaitwa ndani ya Hema kufanya mtihani wangu. Mtihani wenyewe haukuwa mkubwa sana, bali ilikuwa utungaji kwa Kiingereza na kusemezana Kiingereza, kwa sababu mabwana wengi walioianza Company ya Kongwa hawakujua kusema Kiswahili. Kwa bahati njema nilipita nikakubaliwa.

Kazi niliyoanza ilikuwa Karani wa Muster Roll na vipande Time-keeper. Nilifanya katika Offisi hiyo ya Chief Time-keeper pamoja na makarani wengine wawili, mmoja Mfipa na wa pili Mpare. Lugha iliyotumiwa ilikuwa Kiingereza tu, mpaka tutoke ndipo tutumie Kiswahili.

Baada ya mwezi mmoja nilipata uhamisho kwenda Offisi nyingine ya Sanitary Engineer Bwana F. J. Hore. Katika Offisi hii nilikuwa peke yangu tu. Hapa nilitumika kama kazi mbili, Karani na mkalimani, maana watumishi walipokuwa wakitaka kusema na Bwana walinambia mimi, na nilimwambia Bwana Hore; na majibu yake alinambia na kuwaambia watu. Mwendo huu ulikuwa mwema kwa sababu ulinilazimisha mimi kutumia ulimi wangu kila siku kwa lugha ambayo ni ngeni kwangu, kadhalika kusikiliza na kujiendeleza.

Malazi yetu yalikuwa ndani ya mahema. Kila mwanamume aliyeoa alizuiwa kuleta mkewe humo ndani ya kampuni. Waliopendelea kuwapeleka wake zao waliwaweka au kuwajengea mbali huko nje ya kampuni. Kwa hiyo taabu na raha vilishirikiana mkono kwa mkono. Hivyo wasiokuwa na mazoea hayo walishindwa na wengi wao walifuta kazi kwa muda si mrefu.

Mwishoni mwa mwezi Desemba 1947 nilipokea Barua toka Dodoma Bomani. Barua hiyo iliandikwa na Bwana R. W. Smith (D. O.). Alinikumbusha kama bado napenda Kongwa au sivyo. Kwa vumbi jingi la Kongwa na hali ya tabia yake, nilishitukia nimeandika barua kuwa awe tayari kunipokea mwishoni mwa mwezi January, 1948. Kwa kweli ahadi hiyo ilitimia nikarejea Dodoma mnamo 31. 1. 1948.

Nilipokewa na Bwana R. W. Smith kwa furaha akaniweka katika kazi ya kodi kwa mshahara wa Shs 61/= na Kongwa nikaondoka ambapo nilikuwa napata mshahara wa Shs 60/= pamoja na Posho.

## *SURA YA KUMI NA MOJA*

## *KAZI YA KODI TENA NA MAENDELEO MENGI*

Katika tarehe 1 February, 1948 nilaanza kazi ya Karani wa kodi. Kati kati ya mwezi huo nilipelekwa Nondwa. Nilikaa Nondwa mpaka mwezi wa Mei, 1948. Juni nilihamishwa tena na kupelekwa Itisso ambako nilikaa mpaka mwezi Septemba, 1948. Tena Oktoba 1948 nilirudia Nondwa kwa uhamisho.

Mazoea hayo ya uhamaji au kutembea-tembea kama yalikuwa yamenitoka na niliyasahau kabisa kwa muda wa miaka michache iliyopita wakati nilipokuwa nafanya kazi hiyo. Haikuwa vyepesi, lakini kazi mtu anayoijua kujikumbusha ni vyepesi, hivyo mara nilizoea safari safari na uhamisho vile vile.

Nondwa nikahamishwa tena mwishoni mwa mwezi Julai, 1949. Nilikwenda Itisso na Zanka kwa muda tu kwa miezi miwili Agosti na Septemba. Mwishoni mwa mwezi Septemba nilihamishwa nikaenda Kikombo. Niliishi Kikombo tangu Oktoba 1949 mpaka Aprili, 1950. Nilipata uhamisho kwenda Matumbulu kwa Mtemi Luwao, maana kule Kikombo ilikuwa kodi ya 1950 imekwisha. Kwa bahati nilimaliza kodi ya huko mpaka Agosti, 1950.

Katikati ya mwezi Agosti nilipokuwa safarini Matumbulu nilipokea barua ya Bwana D. C. kuniarifu ya kwamba: “Kodi ya Matumbulu imekwisha, kwa hiyo umechaguliwa tena kwenda Kongwa kutoza kodi katika kampuni ya O. F. C. kwa idhini ya Bwana P. C.”. Kwa hiyo nilisafiri kwenda Kongwa mwanzoni mwa mwezi Septemba, 1950.

Nilifikisha barua yangu kwa Bwana D. C. wa Kongwa F. A. Giles nilimpa barua niliyopewa na Bwana Shaw D. C. wa Dodoma.

Nilikaa Kongwa Septemba na Oktoba, 1950. Mwezi Novemba nilikwenda livu yangu ya siku ishirini na nane. Baada ya likizo mnamo mwezi Desemba nilikwenda kutoza kodi Kinyambwa.

Mwanzoni mwa mwaka nilibadilishwa kwenda Dodoma-Nala ambako nilifanya kazi mpaka tarehe 31. 3. 51 nikabadilishwa kutoka katika mamlaka ya Boma kwenda katika mamlaka ya wenyeji kuwa Karani wa Baraza la Rufaani ya Watemi wote wa Wilaya ya Dodoma tarehe 1. 4. 51.

Wakati huu nilikuwa nimechukua masomo mengine kama kujifunza Taipu kama ilivyo kawaida yake na mbio za kupiga Taipu. Hivyo Bwana Shauri mmoja aliyekuwa chini ya D. C. alipendelea sana kama ningefanikiwa kupita mtihani huo. Wakati huo nilikwisha chukua masomo mengine tena kutoka Premier College Nairobi ya "Book-keeping and Accountancy". Niliendelea vizuri sana.

Wakati huo wote cheti changu cha Boma nilikuwa sijapata pamoja na P. F. yangu. Sikupata upesi vyote, maana walisema mambo yote yako mikononi mwa Wakuu wa Dar es Salaam, kama Accountant General kwa ajili ya P. F. na Chief Secretary kwa kusaini Cheti changu.

Baada ya hayo nilipokea Cheti kilichoandikwa hivi:-



TANGANYIKA TERRITORY

**Certificate of Service**

Name of Officer ......... MATHIAS E. MNYAPALA

Position held and Department ......... TAX CLERK, PROVINCIAL ADMINISTRATION. DODOMA DISTRICT.

Period of Service: From ......... 1/2/1948 to 31/3/1951.

Cause of termination of engagement ......... Resigned at own request.

Efficiency ......... Very Good

DOD/5/140
3-10-56

General conduct ......... Very Good.

LABOUR EXCHANGE
KILOSA
KLE/5/117
15-6-54.

Head of Department

Chief Secretary

12/4/1957

Efficiency and General Conduct are assessed as "Very Good," "Good," Fair" or "Indifferent"

G.P.Dsm. S 59246 548 5m

© ROY 2007 (picha)

Fedha yangu ya P. F. nilipata pia baada kupata kwanza Certificate yangu. Basi ikawa mshahara wa Shs 73/= nimeuacha na kuanza mshahara wa Shs 75/= na nyongeza fedha ya gharama ya kuishi. Nikajiona naendelea vizuri na elekeo lenye tamani.

# *SURA YA KUMI NA MBILI*

# *MAENDELEO YA KAZI YA HAZINA YA WENYEJI NA MATOKEO YAKE*

Maendeleo ya kazi yangu katika Hazina ya Wenyeji yakawa mema sana. Kazi niliyoanza ndiyo kuwa Karani wa Baraza la Watemi wote wa Wilaya ya Dodoma. Kwa vile nilikuwa nimechukua masomo yangu ya Taipu niliambiwa na Offisa wangu kuwa sitapata maongezo ya mshahara wangu mpaka nimepita mtihani huo wa Taipu. Wakati huo nilikuwa na mshahara wa Shs 75/= tu. Nilianguka mara 2 mtihani huo. Mnamo tarehe 1. 11. 1951 nikapita.

Wakati huo nilianza shughuli nyingine nyingi. Nilianza kukamilisha habari za uandikaji wa kitabu cha kwanza cha "Historia mila na Desturi za Wagogo". Punde si punde, nilishauriana na watu wengi na mabwana wa Serikali Kuu kuanzisha Gazeti moja jipya la nchi ya Ugogo. Kwa majadiliano lilichaguliwa jina la "WELA" ndilo lililokubaliwa na wengi likaanzishwa mwezi Oktoba, 1952. Na Mtengenezaji wa Gazeti "WELA" akachaguliwa mimi mwenyewe.

Kushinda kwa mtihani huo wa Taipu kulinifanya niongezwe mshahara wangu toka Shs 75/= nikaongezwa Shs 20/= zikawa Shs 95/=. Nililipwa vile vile malipo ya nyuma tokea Septemba 1951. Nilipofika mwaka mpya 1952 nilipata maongezo Shs 5/= zikawa Shs 100/=. Basi kwa hivyo nilijiona na maendeleo mema yananikabili, na watawala wangu wote na mabwana wa Serikali nikawa na upepo nao mwema.

Kwa bahati njema mwezi wa Machi, 1952 nilipachikwa mzigo mwingine kwa vile Katibu wa Hazina ya Wenyeji alitoka (N. A. Secretary) nilichaguliwa mimi. Badala ya jina la Secretary nikaitwa N. A. Staff Clerk. Hivyo niliongezwa Shs 20/= nikawa na 120/= kwa mwezi. Hivyo kazi nilizozifanya zikawa zimeongezwa zaidi na mamlaka yote ya utawala wa wenyeji yakawa mikononi mwangu bila kinyume, upepo na nuru vikazidi kukua na kuongezeka na walio viongozi wangu mnamo mwaka huo 1952 nilichaguliwa tena na Halmashauri ya Social Welfare Centre kuwa mtunza Hazina yao kwa Dodoma.

Mwanzoni mwa mwaka 1953 ndio ulikuwa mwaka wa bahati njema sana na mbaya kwangu. Niliongezwa Shs 55/= nikawa na mshahara wa Shs 175/= kuanzia Januari 1, 1953. Wakati huu sikuwa N. A. Staff Clerk, bali Secretary mzima, na kazi ya Karani wa Baraza la Watemi nikamwandika mtu mwingine mimi nikashika madaraka makubwa na uongozi wa Gazeti letu, na mengineyo mengi. Lakini jicho la kipanga halipendi kuona usitawi wa vifaranga vya kuku ugani. Na kila mara utukufu wa mtu huchukiza miongoni mwa nyoyo za watu wa roho chafu.

Mnamo tarehe 25. 3. 53 Bwana Shauri (D. O. I.) aliondoka kwenda livu kubwa. Na mwishoni mwa mwezi Aprili, 1953 District Commissioner wangu akaenda livu kubwa vile vile. Watafutao vipengee walipata nafasi hapo.

Tarehe 3. 6. 53 nilipata kufikiwa na Bwana Rashidi M. Kawawa kwa ajili ya utafutaji wa Hadithi ihusikanayo na upiga picha za Sinema ya Kiafrika. Kwa vile nilikuwa mimi ndiye mtoa habari kwa Radio (Radio News Correspondent) na mtengenezaji wa Gazeti la “WELA” nilichaguliwa mimi kumshauri Bwana Kawawa hata akafanikiwa kazi yake. Na kwa vile nilikuwa nimekwisha tunga kitabu changu cha “Habari za Ugogo” likachaguliwa jina la “CHALO” ikawa Sinema hiyo ikaitwa “CHALO, AMERUDI”, toka katika kitabu hicho.

Kwa bidii yote nyingi iliishia hapa, ikawa kazi yangu imeishia tarehe 31. 7. 53. Labda kwa kutokuwa na elimu ya kutosha, ama bahati ina ukingo wake mambo yangu yaliharibikia. Walionipenda wakawa na masikitiko makuu na waliochimba shimo wakapiga vigelegele na kufunga vibwebwe.

Wakati huo nilikuwa nimejipatia vyeti kama viwili vya aina mbali mbali na maendeleo makubwa mno. Hivi ndio vyeti nilivyojipatia wakati nilipokuwa N. T.:-


Voice of Prophecy Bible School
CERTIFICATE of AWARD
This is to Certify that Nathias E. Mnyampala
has completed in a satisfactory manner our Bible Doctrines Course of Study.

A MORE SURE WORD OF PROPHECY
2 Pet 1.19

25th January, 1952.
G. S. Stevenson
Director.

© ROY 2007 (picha)

Cheti hiki nilipata kwa vile nilikuwa nikitangatanga kutafuta elimu ya aina nyingi. Hii nilichukua kwa kusomea Biblia. Shabaha yangu kuu ni kujiendeleza na Kiingereza kwa kusoma na kuandika. Masomo hayo kwa kweli yaliniendeleza sana na kupata kujua mambo ya aina nyingi na zenye asili mbali mbali.

Basi baada ya hii nikapata ile ya Taipu iliyoandikwa hivi:-



CENTRAL PROVINCE

DISTRICT OFFICE,
DODOMA

Ref. No. 3/8/17.

15th March, 1952.

CERTIFICATE.

I certify that Mathias Mnyapala, Court Clerk, Native Treasury Dodoma has passed his typewriting test with a speed of 32 words per minute.

DISTRICT COMMISSIONER.

© ROY 2007 (picha)

Mafunzo haya ya Typewriting nilichukua kusomea Touching method.

Kwa bahati nilipita maneno yaliyokuwa yananilazimu ni 25 kumbe nikapata 32 kwa dakika baada ya kuanguka mara 2 hivi mbele ya Boma.

Mbio za sakafuni huishia ukingoni nikarudi kuchunga bata na kebehi nyingi zanifuata. Dunia ni mti mkavu kila kiumbe hukutana na machungu. Kuna siku za vicheko na vigelegele, halafu siku za huzuni vilio na mahangaiko ya moyo na majuto kwani yote hayo yaliumbwa. Bali mwanamume hakati tamaa ikiwa kufa hakujakufikia bado kaza moyo na nia mbele utazame upeo wa maisha yako mengine yaliyobaki. Kwani Bwana Mungu ni mwenye huruma. Kitamu hukigeuza kiwe kichungu, na kichungu kikageuka asali – bali safi nia yako kila mara kuwa nyeupe mbele ya Mungu na kwa wenzio.

# *SURA YA KUMI NA TATU*

# *MAJUTO HUJA NYUMA*

Baada ya mgogoro na kuacha kazi kwangu katika Hazina ya Wenyeji nafasi yangu ilibaki tupu haikupata mtu mpaka Bwana D. C. wa zamani aliporudi toka katika livu yake. Bwana huyu ni Mr. J. T. A. Pearce. Alikuta mambo yamechafuka na kuharibika kabisa. Masikitiko yake kwa ajili ya kazi yangu yalimwingia moyoni. Hakuacha aliandika barua kwa Bwana P. C. Mr. L. M. Heaney, nae alikubali kuwa nirudie kazini.

Mnamo tarehe 10. 5. 54 kulikuwa na mkutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma yalizungumzwa juu ya kazi zangu na Halmashauri nini wanafikiri? Hivyo kila Mtemi na Halmashauri walikubali na kupendelea nirudi kazini, maana kila mmoja alijua kwa nini machafuko hayo yalitokea. Basi ikawa lazima nirudi kazini, hasa nifungue tena Gazeti la "Wela" ambalo lilikuwa limefungwa na halina kiongozi na mtengenezaji.

Mnamo mwisho mwa Mei, 1954 niliitwa na Bwana D. C. nami nilihudhuria lakini mashauri yetu hayakumalizika siku ile ile, yakaahirishwa mpaka tarehe 9. 6. 54 baada ya Bwana D. C. kurudi kutoka safarini. Tarehe hiyo kweli tulikutana nae, na niliambiwa "Umechaguliwa tena na Halmashauri ya Wilaya urudie kazini kwako, na zaidi hasa uendeshe Gazeti lako kama zamani". Mimi niliuliza habari za malipo ya mshahara.

Na nilijibiwa kuwa "Utaanza upya tena, baada ya muda kupita ndipo utarudishiwa mshahara wako wa Shs 175/=". Basi nilivyosikia vile nilijiona upendo au uchaguo huo haukuwa na stahili kwangu, basi nilitafuta moyoni sana ili nigundue kinachonielekea. Hivyo nilimjibu kuwa "Bado nafikiri halafu nitatoa majibu kamili".

Uchaguo wa moyo wangu ukawa nielekee kwanza pande za Boma la Kilosa. Hivyo niliondoka tarehe 11. 6. 54 Ijumaa na abiria ya usiku na nilifika alfajiri Kilosa 12. 6. 54. Siku ya Jumaatatu 14. 6. 54 nilifika Bomani Kilosa kuonana na Bwana Labour Officer. Kwa bahati nilikuta iko nafasi anatakiwa Karani mmoja wa kupiga mashine kule Ilonga Agricultural Department ambayo yajulikana kwa jina la "Colonial Agricultural Insecticide Research Unit". Nilifika huko, lakini tulishindana na mambo ya mshahara kuwa nipewe Shs 80/= plus Cost of Living Allowance. Hivyo nilishindwa, nikarudi tena Bomani huko ndiko nilikoambiwa nafasi nyingine ya Karani wa kupiga Taipu kwa shamba moja huko Kimamba liitwalo Antoniou Sisal Estates Ltd., Kimamba. Nilianza kazi kule tarehe 16. 6. 54, nikaanza maisha mapya ya nchi za ugenini, nikaacha maskanini Dodoma. Mnamo tarehe 14. 7. 54 nikapokea barua toka nyumbani kwa tanzia ya kifo cha mama mzazi na hivyo ikawa lazima nifanye inavyopaswa kutimiza wajibu wa vifo kule nyumbani.

# *SURA YA KUMI NA NNE*

## *KAZI UGENINI, NA KURUDI DODOMA*

Kazi yangu ya Karani wa kupiga Tapureta katika Antoniou Sisal Estates Ltd., Kimamba niliendelea nayo tangu 16. 6. 54 hiyo mpaka tarehe 22. 11. 54 ambapo niliitwa na District Traffic Superintendent wa E. A. R. & H. Dar es Salaam ambako nilikuwa nimepeleka maombi yangu ya kazi hii ninayojua. Mwito huo ulikuja pamoja na Nauli yao nilikwenda Dar es Salaam mnamo tarehe 29. 11. 54 na nilipokewa na mdogo wangu afanyaye kazi huko katika kundi la Polisi. Tarehe 30. 11. 54 nilionana na wakuu wa Idara hiyo nikajaribiwa, kwa bahati niliweza kama inavyotakiwa. Malipo yao ya mshahara kwa mji kama ule nilishindwa, nilipewa nauli yangu kurudi Kimamba.

Niliondoka Dar es Salaam tarehe 7. 12. 54 nilifika usiku Kimamba, na tarehe 9. 12. 54 nilaanza kazi yangu ya Karani wa kupiga Taipu kule Ilonga Estates, Rudewa Estates Ltd., Kimamba. Makao ya hapa yalinipendeza kidogo kuliko kule Kimamba kwa Antoniou Sisal Estates Ltd., kunifaa kwangu kuwa nilifanya kazi na mke wangu aliendesha Biashara ya kupika pombe ya kuuza kilabuni. Lakini mzee wangu alikuwa amekuja kama mara tatu hivi na haja yake kunishauri kuwa nirudi Dodoma kufanya kazi huko. Maana ni taabu kwake kunifuata mara kwa mara huko mbali hivyo hali nae ni mzee sana. Mashauri hayo yaliambatana na ukiwa aliokuwa nao baada ya kifo cha mama mzazi. Ikawa lazima nitoe barua kwa mabwana wangu niache kazi na kurudi nyumbani kumwangalia mzee.

Mnamo tarehe 15. 8. 55 nilipeleka barua ya kuacha kazi, barua iliandikwa kutaja tarehe 30. 9. 55 ndio mwisho wa kazi yangu. Bwana John A. Salt Manager wa shamba hilo alisikitika sana kwa nini niache kazi? Lakini sababu zangu kama nilivyoeleza zilimtuliza. Kabla ya kuacha kazi niliandika barua kwa Bwana D. C. Kilosa kuomba ruhusa kupata Cheti cha Kilabu ya Pombe kule Stesheni ya Mkata. Maombi hayo nilifanikiwa niliposaidiwa na Mtawala wa Usagara Mndewa Kutukutu III wa Masanza Kilosa nikapewa cheti kwa gharama ya Shs 85/= kila mwezi kuanzia 1. 10. 55. Cheti hiki na kazi zote nilikabidhi mke wangu kuendesha Kilabu, nami nilirudi huko Dodoma. Mara kwa mara nilikwenda mwangalia huko Mkata anavyoendeza kazi yake.

Kilabu ilifungwa mwezi Desemba 1955 nami nilirudi Dodoma kabisa nilipitia Mpwapwa kwa maagizo ya Bwana Mwalimu wa Dodoma Bwana G. N. Shann P. E. O. aliponituma kwenda kufanya mashauri ya kitabu changu cha "*Hadithi ya mpakuaji wa asali na wenzake wawili*". Mashauri yangu kule Mpwapwa yalimalizwa mapema nikapewa Gari na Bwana Cameroon Headmaster wa T. T. C. kunifikisha Gulwe Stesheni. Mnamo tarehe 24. 12. 55 jioni nikapata Gari la Jumaamosi alfajiri kufika Dodoma mnamo Christmas 25. 12. 55 kungojea siku ya 1. 1. 56 kuanza kazi yangu katika Idara ya Water Development and Irrigation Department Dodoma. Na kweli tarehe hiyo 1. Januari 1956 nilianza kazi yangu Typist Clerk.

Wakati huo nilikuwa nimepata vyeti vingine vya kazi kutoka katika Antoniou Sisal Estates Ltd., Kimamba, na Ilonga Estate, P. O. Kimamba kama:-



ANTONIOU SISAL ESTATES LTD.
KIMAMBA
TANGANYIKA TERRITORY.

No 444

Kimamba, 22nd November 1954

CERTIFICATE OF SERVICE

This is to certify that MATHIAS MNYAPALA

has completed four cards in our service as a typist - clerk

He leaves today on reduction

His work has been Good

DO7/5/140
3-10-56

For and on behalf of
ANTONIOU SISAL ESTATE LTD.
Manager/Field Ast,

© ROY 2007 (picha)

Baada ya hii niliyopata toka Antoniou Sisal Estates Ltd. ikawa nimepewa tena nyingine toka kule Ilonga Estate (yaani shamba la Tawi la Tanganyika Cotton Company Ltd. ya Morogoro) ni kama ilivyoandikwa hapa:-



# ILONGA ESTATE

DIRECTORS:-
D. PARKER
W. D. SCOTT
H. W. O. JENKINS
D. P. ELPHICK
~~J. SCOTT-BARRETT~~ E. COLLINGS

REGISTERED OFFICE AND SECRETARIES
TANGANYIKA COTTON CO. LTD.
MOROGORO

TEL. ADDRESS: "RUDEWEST"
CODE: BENTLEY

Rudewa Estates Ltd.
P.O. Kimamba
Tanganyika Territory

30th September, 1955

DOD/5/140
3-10-56

**TO WHOM IT MAY CONCERN.**

This is to certify that bearer Mathias E. Mnyampala has worked on this Estate as a Typist for the past 10 months.

In addition to his duties as Typist he has been engaged in keeping Cost Schedules etc.

I have found Mathias always a willing worker and can recommend him to anyone wanting a Good Typist/Clerk.

He leaves at his own request owing to the death of one of his parents.

ILONGA ESTATE
Rudewa ~~Estates~~ Ltd
Manager.

© ROY 2007 (picha)

# *SURA YA KUMI NA TANO*

# *KARANI KATIKA IDARA YA WATER DEVELOPMENT DODOMA*

Katika tarehe 15. 11. 55 nilifika na vyeti vyangu mbele ya Bwana Labour Officer Dodoma waliokuwa wanataka Karani. Mnamo tarehe 17 Novemba, 1955 Labour Officer aliniita kwamba imetokea nafasi ya kutakiwa Typist mmoja katika Idara ya maji Dodoma. Baada ya kufika nilipewa majaribio kama nafaa au hapana, maana Idara hiyo ilitaka Karani wa Taipu aliye hodari. Bwana Labour aliridhika akanipa karatasi kupeleka katika Idara hiyo ya usitawisho wa maji siku ile ile.

Nilifika katika Idara hiyo kama saa 4 hivi, nao walinipa majaribio yao juu ya kazi hiyo, nao waliridhika nami wakaniuliza mshahara gani nilikuwa napata huko nilikokuwa nafanya kazi wakati uliopita. Niliwatajia mshahara mbalimbali lakini ulio wa juu zaidi ulikuwa Shillingi 175/= kwa mwezi. Niliulizwa darasa, hapo niliweweseka tu nikataja darasa la nane Kiingereza, wakaridhika. Nilijibiwa kwamba "Tunaandika barua kwa Director of Water Development and Irrigation Department Dar es Salaam, akikubali uanze na mshahara wa Shs 170/= tutakuandika. Njoo kusikia majibu yake mwishoni mwa mwezi huu". Basi mimi niliondoka. Kwa bahati saa nane hiyo hiyo niliitwa na Bwana G. N. Shann, Provincial Education Officer, Dodoma kwa ajili ya kitabu changu nilichotunga cha "*Hadithi ya mpakuaji wa Asali*". Katika kuendelea na mazungumzo ya mpango wake, na jinsi kitabu hicho kilivyokubaliwa kikapigwa chapa na kutumiwa na Walimu katika mashule. Alisema maoni hayo yalitolewa na mabwana wa T. T. C. Mpwapwa baada ya kusoma nakala yake.

Baada ya hayo aliniambia kwamba: “Nitakupa barua ufike huko Mpwapwa wanahitaji mwende kuonana ili mkamilishe mpango wa upigaji chapa kwa kitabu hicho, ni vema zaidi”. Nilikubali akaniandikia barua na akanipa ile nakala ya kitabu changu.

Kabla ya kuondoka aliniuliza kuwa wapi nafanya kazi sasa? Nami nilimwambia: “Kwa sasa sina kazi na hivi natoka Water Developement Department wanataka Karani wa Taipu mmoja, lakini nimeambiwa nije mwisho wa mwezi kupata majibu kamili”. Alinijibu ya kwamba “Kwa kuwa nakufahamu sana tangu ulipokuwa Hazina ya Wenyeji, na jinsi juhudi yako ilivyo, ningependa kama ungekuwa mtumishi katika Idara hii ya Elimu. Mwishoni mwa mwezi ujao Karani wetu mmoja anaacha kazi kabisa. Kama unapenda mimi nitaandika barua kwa Mkuu wa Idara hii Dar es Salaam akiniruhusu kujitafutia Karini mwenyewe itakuwa wewe”. Mimi nilikubali, nae akasema “barua naandika leo hii, njoo mwisho wa mwezi kusikia majibu”. Basi baada ya kutoka hapo Bwana Liwali wa Dodoma akaniambia kwamba wao wanatafuta Typist mmoja katika Dodoma Town Council mwenyeji akasema angefurahi sana kama ningekuwa nimi.

Niliondoka Dodoma kwenda kuangalia mke wangu huko Mkata na kuona kazi yake jinsi inavyoendelea. Nilikaa huko hata Desemba ilipofika nilifika Dodoma tena kusikia majibu. Nilionana na Bwana Mwalimu alisema: “Atakuja Karani mwingine toka Hedkwata, lakini nasikitika nitafanya nini”. Nilipofika Water Development nilikuta majibu yametoka kwa Director anasema: “Siwezi kukubali kumpa Karani yeyoye mshahara wa Shs 170/= bila kwanza kuona Cheti chake cha Shule cha darasa la kumi kama alipita mtihani wa Serikali, kama hana lazima aanze na mshahara wa Shs 120/= na kutazama maendeleo yake kama miezi 6 halafu nitamfikiria baadaye”.

Barua hii niliposomewa nilipata masikitiko makubwa sana. Lakini nitafanya nini, kumbe mzee nae anang'ang'ania tu kwamba nipate kazi hapa Dodoma? Hivyo nilikubali mshahara huo wa 120/= kwa mwezi. Baada ya ukubaliano walimwandikia barua Director kwamba: "Tumekubaliana kwa mshahara wa Shs 120/= na kazi itaanza tarehe 1. 1. 1956; na huyu tuliyekuwa nae tumempa barua ya kuacha kazi kwamba hafai. Kazi yake itaishia tarehe 9. 1. 56. Kwa hiyo tupelekee mapema Departmental Warrant ya Karani huyu mgeni kwa ajili ya mshahara wake". Nilikwenda Mkata kumwangalia mke wangu.

Katika tarehe 16 January 1956 Mkuu wa Idara hii aliandika barua kwa Divisional Engineer wetu wa Dodoma kwamba: "Nipe taarifa ya Bwana Mathias E. Mnyampala, kiasi cha elimu ya madaraka yake na ujuzi mwingine kwa kazi alizofanya baada ya masomo yake. Haiwezekani kwa mimi kukubali mshahara wa Shs 120/= kuwa ni sawa na elimu yake au hapana. Basi habari zake darasa gani alifika kadhalika na kazi gani alifanya kwanza nipe majina na mahali alipofanya. Baada ya kujulishwa habari hizo nitakupa hakika yake".

Baada ya kusomewa barua hiyo nilikonda mwilini. Mawazo yangu yakawa mengi mno. Elimu ya leo mpaka uwe na Cheti cha kuacha shule na madarasa uliyopita, mimi sikuwa na Cheti cha Shule, bali vyeti vya kazi nilikuwa navyo na vya elimu fulani fulani niliyojifunza juu juu tu.

Hivyo walitaka vyeti vyangu vyote, na kusema isipokuwa cha shule tu sina, lakini niliacha darasa la nane, (kwa kutaka nifanikiwe). Wakati wote huu nilikuwa nafanya kazi, lakini mshahara haujajulikana baado.

Offisa wangu aliandika barua kwao tarehe 23. 1. 56 na kutaja vyeti vyangu vya kazi kimoja kimoja, sifa yake, na mahali nilipofanya na tarehe ya kuacha. Isipokuwa tu sina Cheti cha shule nilisoma zamani 1936. Baada ya kutaja sifa za vyeti hivyo alitia mkazo sana na kusifia sana kazi zangu zinavyokwenda, na hapana budi ningepata mshahara mwema zaidi kuliko huo na 120/= zikipunguzwa mtu huyu atakimbia na itakuwa hasara kwetu. Maana ni vigumu sana katika mji wa Dodoma kumpata Karani Mwafrika wa Taipu aliye hodari sana kwa upesi sana.

Mpaka mwisho mwa mwezi majibu hayajaja sikupata mshahara mpaka tarehe 9. 2. 56 ndipo tulipopokea simu ya kusema: “Mshahara wake ni Shs 160/= kujibu barua yako ya 23. 1. 56”. Hata tarehe 13. 2. 56 Chief Secretary to the Government akaandika barua yake ya ukubalio (In the Lower Clerical (b) Scale), kwa mshahara huo 160/= katika Temporary muda wa miezi 6 baada ya hapo na sifa au kazi ikiwa njema ndipo niandikwe mtumishi wa daima.

Tarehe 1 July, 1956 nilipata maongezo ya mshahara wangu zikawa Shs 173/75 Clerk “General Division”. Kutokutimiziwa ahadi yangu niliacha kazi katika Idara ya maji.

Wakati nilipoacha kazi tarehe 20/9/1956 nilikwenda jitafutia shamba Zuzu kulima. Hapo nilipata Hati ya kuacha kazi (Certificate of Service) kama hivi hapa chini ifuatavyo:-



*Telegraphic Address:* "Tributary" Dodoma
*Telephone Nos.:* 53 and 54
In reply please quote

Ref. No. 2/27/17.

DEPARTMENT OF WATER DEVELOPMENT AND IRRIGATION,
DIVISIONAL ENGINEER,
DODOMA

20th September, 1956.

TANGANYIKA TERRITORY

DOD/5/140
3-10-56

- CERTIFICATE OF SERVICE -

Name of Officer: MATHIAS E. MNYAMPALA.

Position held and Department: TYPIST
WATER DEVELOPMENT & IRRIGATION DEPT. DODOMA.

Period of Service. From: 1/1/1956 to 20/9/1956

Cause of Termination of Engagement: RESIGNED AT OWN REQUEST.

Efficiency: GOOD

General conduct: GOOD

Divisional Engineer
Water Development
DODOMA

DESIGNATION.

Right thumb of bearer or Signature.

Efficiency and General Conduct assessed are "Very Good", "Good", "Fair", or "Indifferent"

© ROY 2007 (picha)

## *SURA YA KUMI NA SITA*

## *KARANI KATIKA IDARA YA KILIMO DODOMA*

Ingawa nilikusudia kuendesha kilimo kule karibu na Stesheni ya Zuzu umbali wa maili 9 toka Dodoma mjini, aliyezoea kazi ni shida sana kukataa kazi imtokeapo mbele ya macho yake. Ilikuwa ni Jumaapili tarehe 4/11/1956 Karani wa Mkuu wa Idara ya Kilimo wa Jimbo la kati alifika nyumbani kwangu kuniambia kwamba yeye anatazamia kwenda likizo kwao Unguja, nao hawana Karani mwingine Mwafrika wa kushika mahali pake. Karani huyo jina lake alikuwa ni Athmani Ibrahim. Alisema Afisa wake alikuwa amearifiwa kwamba mimi nilikuwa nimeacha kazi katika Idara ya Ustawisho wa Maji, hivyo Afisa wao alinihitaji nikamshikie Bwana Athmani kazi yake kwa muda wa mwezi mmoja tu. Mimi nilitoa udhuru wangu lakini alizidi kuninasihi nikamshikie mpaka atakaporudi.

Jumaatatu tarehe 5/11/1956 nilifika katika Afisi ya Kilimo na nilimkuta Bwana Shamba wa Jimbo la kati Bwana K. Johansen. Bwana huyu alikuwa ananijua tangu nilipokuwa Hazina. Baada ya kuonana naye aliniomba nishike kazi ya Karani wake kwa muda wa siku thelathini tu. Nilimwambia shida zangu za mashamba na pia nilikuwa na madai ya ng'ombe kumi huko Bahi. Bwana Johansen aliniahidi kuwa pindi ninapotaka kwenda huko nitapewa ruhusa ili niende kwenye shughuli zangu. Tulikubaliana na Bwana huyu kwa kuanza kazi na nilianza kazi siku ile ile ya tarehe 5/11/56. Bwana Athmani Ibrahim Karani huyo aliondoka kwenda Unguja.

Baada ya mwezi mmoja hivi Karani huyu hakurudi lakini alipeleka barua akisema kuwa hakuwa na nafasi, aliomba kuongezewa siku kumi zaidi. Baada ya siku hizo alirejea kazini kwake. Afisa wa Kilimo aliniomba kuwa afadhali nikamilishe tena mwezi wa pili ndipo nitakapoondoka. Hivyo ikawa nimesonga tena mwezi wa Desemba, 1956.

Baada ya kuendelea na kazi hiyo ilipofika tarehe 22/12/56 Bwana Athmani Ibrahim aliomba ruhusa ya kwenda kulia Sikukuu ya Christmas huko Kimamba kwa wakweze. Aliruhusiwa. Ahadi ya kurudi Afisini ilikuwa tarehe 27. 12. 56 lakini Karani huyo hakurudi kama tulivyotazamia. Ilipofika saa 8 mchana tulipokea simu yake akisema kuwa basi yeye kazi hataki, mshahara wake uwe ndiyo badala ya Notisi yake ya kuacha kazi.

Nami ikawa nimemwambia kuwa: "Na mimi kazi basi kwani shughuli zangu zilizonifanya niache kazi huko kwenye Idara ya Maji zilikuwa zinaningoja". Bwana K. Johansen Afisa wa Kilimo alinisihi kuendelea na kazi mpaka atakapopata Karani mwingine. Ukaidi si maungwana, nilikubali kuendela na kazi. Karani mwingine hakupatikana nikaombwa kuendelea moja kwa moja kazi. Wakati huo nilikuwa nalipwa mshahara wa Shs 176/= kama Karani wa daraja la chini. Niliendelea na kazi yangu kwa vizuri sana nikapata sifa njema sana.

Mnamo 1/5/1958 nilichaguliwa na D. C. kuwa Diwani wa D. D. C. na 1/1/1959 nikachaguliwa tena kuwa Halmashauri wa elimu Dodoma. Baada ya kazi yangu nikawekwa tena kuwa mfasiri mashuhuri makala nyingi za kilimo zilizoandikwa Kiingereza kuzifasiri katika lugha ya Kiswahili ili kuzigawa kwa wakufunzi wa kilimo na kuwagawia wakulima. Mpaka mwaka 1960 Januari nikawa na shahara wa Shs 208/=.

Tangu hapo sijaacha tena mpaka leo hii.

# *SURA YA KUMI NA SABA*[4]

# *KAZI YA ULIWALI MPANDA*

Baada ya kuendelea na kazi ya ukarani katika Idara ya Kilimo siku moja niliposoma Jarida la Serikali niliona tangazo la nafasi ya kazi ya uliwali huko Mpanda. Nakumbuka lilikuwa la tarehe 16 Novemba, 1959.

Nilipeleka maombi yangu kwa Bwana P. C. wa Tabora kupitia mikononi mwa Mkuu wetu ambaye jina lake aliitwa Brookbank. Barua yangu ilipitia mikononi mwa Bwana D. C. wa Dodoma Bwana Aers. Barua hiyo aliipeleka kwa njia ya Siri (Confidential) na mapendekezo yao.

Nilikaa sana bila kupata majibu tangu Novemba 1959 mpaka Februari 1960 nilijibiwa kuwa nimekubaliwa na niende Mpanda haraka. Mshahara wangu ulikuwa Shs 218/75.

Nilisafiri kwenda Mpanda tarehe 28/2/60 toka Dodoma na nilifika Mpanda tarehe 29/2/60. Tarehe 1/3/1960 nilianza kazi ofisini katika Mahakama ya mji wa Mpanda. Ingawa nilianza kazi na mshahara wa Shs 218/75 mwaka 1961 uliongezeka na kuwa Shs 230/= na mwaka 1962 kwa kufuata Ripoti ya Kadu nilipata mshahara wa Shs 266/=.

Kazi yangu ilikuwa kuutawala mji wa Mpanda na sehemu zote za Kampuni ya Madini Mpanda. Cheo cha Liwali au Jumbe Mkuu wa Mpanda ilipofika mwezi wa Septemba 1962 nikashika kazi ya Uhakimu tu utawala ukawa mikononi mwa Wizara ya Utawala.

---

[4] Inaandikwa “SURA YA KUMI” katika mswada (mhariri).

Nilipata bahati ya kuandika vitabu vingi – kama vile *Diwani ya Mnyampala, Waadhi wa Ushairi, Utenzi wa Enjili, Mbinu za Ujamaa, Kito cha Hekima* na *Taaluma ya Kiswahili,* na kadhalika.

Nilihama Mpanda tangu 16/5/1963 kuja Dar es Salaam nikawa Hakimu wa Temeke kisha nikaja Kariakoo tangu 1/7/1963 na kuwa Mkuu wa Mahakimu wengine. Wakati huo nikawa na mshahara wa Shs 350/= na mwaka 1964, Julai nikapata Shs 500/=. Grade III.

## *SURA YA KUMI NA NANE*[5]

## *KUWA KADHI WA DAR ES SALAAM*

Nilikuwa na kazi nyingi Kariakoo na nilijipatia sifa njema. Tangu tarehe 1/4/1966 nikahamishwa Kariakoo kuja Ilala "A" ambapo ni Mahakama ya Kadhi inayoshughulika na Mirathi, Ndoa na Talaka kufuata sheria za Dini ya Uislamu. Kusema kweli ni mara ya kwanza kukaliwa na Mkristo. Wakati huu nikipata mshahara wa Shs 550/=. Kwa hakika kazi hii ya Kadhi ilitofautiana kidogo na ile ya zamani. Kazi zilikuwa ni zile zile bali aliitwa Hakimu Mkuu badala ya Kadhi moja kwa moja kama zamani.

---

[5] Inaandikwa "SURA YA KUMI NA MOJA" katika mswada (mhariri).

Kwa muda wa miezi 8 hivi nilipata uhamisho kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma katika Mahakama ya mjini. Baada ya kuarifiwa uhamisho nikapata maongezo ya mshahara wangu kuwa Shs 740/= kwa mwezi tangu 1/9/66. Hapo ikawa nimewekwa katika (Grade II) Daraja ya Pili. Uhamisho wangu niliarifiwa niondoke tarehe 15/11/66 na ilibadilishwa na kuwa niondoke tarehe 30/10/1966.

Kwa vile mimi ni Rais wa Chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA) Halmashauri Kuu ya UKUTA ilifanya tafrija ya kuagana nami mnamo tarehe 29/10/66 ndani ya Jengo la Chuo Kikuu cha Elimu kwa Watu Wazima. Tafrija hiyo ilifana sana. Halmashauri Kuu iliandaa vinywaji baridi na nilipewa zawadi ya saa ya mezani ili nifikapo Dodoma niikumbuke Halmashauri Kuu na nikumbuke shughuli zake za mara kwa mara zikumbushwazo na saa. Niliondoka mimi mke wangu na wanangu kwenda Dodoma Jumaapili 30/10/66 na kufika Dodoma alfajiri ya 31/10/66, na hapo nilipokelewa vizuri sana na wanachama wa UKUTA wa Tawi la Dodoma.

## *SURA YA KUMI NA TISA*[6]

## *KARII WA MAHAKAMA KUU*

Uhamisho wangu wa kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma ulitimia kama nilivyopelekwa na wakubwa wenyewe wa kazi yangu. Hapo nilipata bahati njema ya kushughulika na mambo pia binafsi. Jengo langu nililoanza tarehe 14/4/64 lilipata bahati ya kuendelezwa na likawa limemalizika mnamo mwaka 1967.

---

[6] Inaandikiwa "SURA YA KUMI NA MBILI" katika mswada (mhariri).

Mnamo tarehe 23/4/68 nilipokea simu kutoka Mahakama Kuu Dar es Salaam ikiniambia niondoke mara moja kuhamia Dar es Salaam. Ni lazima niwe tayari kuwasili Dar es Salaam mapema mnamo Juma la kwanza la Mei 1968 kwa uhamisho.

Hakika nilijiandaa kusafiri kwenda Dar es Salaam kwa uhamisho huo, lakini kwa bahati mbaya njia zilikuwa zimefungwa. Niliondoka Dodoma tarehe 4/5/68 Jumaamosi kwa njia ya Arusha – Moshi – Same – Korogwe mpaka Dar es Salaam. Nilifika Dar es Salaam tarehe 5/5/68 na nilihudhuria Mahakama Kuu mnamo 6/5/68.

Wakati nilipoondoka Dodoma sikujua nakwenda kufanya kazi gani, na hasa nilifikiria kuwa ni kazi zangu zile zile tu za Uhakimu wa Mahakama za Mwanzo. Fikira zangu na matokeo yake vilikuwa tofauti kabisa. Nilipofika nilikuta Msajili wa Mahakama Kuu hayupo yuko safarini. Nilipokelewa na Bwana M. U. M. Minja kwa niaba ya Msajili wa Mahakama Kuu. Bwana Minja aliniambia kuwa “umechaguliwa na Bwana Msajili kushughulika na mambo ya kutafsiri kazi za Majaji kwa hapa kwenye Mahakama Kuu”. Mimi nilimjibu kwamba “kazi ya kutafsiri ni ngumu sana. Inataka mtafsiri usipoteze maana ya neno la asili na kulinda ukamilifu wake. Vipi? Mbona mimi si hodari sana wa lugha ya Kiingereza?

Nitafsirije ili kukamilisha hayo yawe sawa?" Bwana Minja alinijibu kuwa "Tuna imani kubwa kwamba hutashindwa kutafsiri Kiswahili kwa Kiingereza na Kiingereza kwa Kiswahili. Ingawa hutatafsiri kwa Kiingereza fasaha sana lakini Majaji wataelewa ni nini maana yake yaliyotafsiriwa kutoka katika Kiswahili kuja kwenye Kiingereza". Katika majadiliano hayo mimi nilikubali lakini niliwaomba nisije nikapewa kazi ya kutafsiri Mahakama kwa Majaji kama mkalimani kwani kwa usemi ulimi wangu mzito na kutosikia upesi upesi na kujibu upesi upesi. Maombi hayo yalimngojea Bwana Msajili.

Bwana Msajili aliporudi tulionana naye akanifikishia madhumuni niliyoitiwa hapo. Mimi nilijitetea juu ya ujuzi wangu ambao ni mdogo juu ya lugha ya Kiingereza. Naye aliniambia vile vile kama Bwana Minja alivyoniambia. Alikubali ombi langu la kutoingia Mahakamani kwa Majaji kuwa kama mkalimani. Hapo nilifurahi kidogo, kwani tafsiri zangu zitakuwa za kuandika tu.

Baada ya hapo nilikabidhiwa majalada yote yanayotoka kila upande wa Tanzania kwenye Mahakama za Mwanzo kuja kwa Majaji kwa Rufaani. Ikawa lazima nitafsiri jalada zima kutokana na maandishi yote ya Mahakama za Mwanzo na Hukumu zao za Kiswahili kuwa katika Kiingereza na sababu za waombaji Rufaani. Kwanza kazi hiyo ilikuwa ngumu sana kwangu kila nikitafsiri nakuwa na wasiwasi kufikiria kuwa sijui kama Majaji wataelewa tafsiri zangu vizuri au watagomba sijui!

Lakini kwa bahati nzuri niliambiwa tafsiri zangu nzuri zaeleweka vema haidhuru ufasaha (Grammar) wake haukukamilika kama wanachuoni walivyo lakini tafsiri zangu nzuri kwa jumla. Hapo niliondoa wasiwasi, nikajitahidi sana hata wakati wengine huambiwa kuwa "Jalada hili linatakiwa leo hii hii liwe limekwisha tafsiriwa na kukabidhiwa Jaji fulani". Hushika Jalada hilo na hulitafsiri haraka sana na mara Jaji aliyelihitaji hukabidhiwa bila kuchelewa. Ama kwa kweli Mungu akikupa kazi fulani hukupa pia na uwezo wa kutimiza kazi hiyo.

Wakati niliposhika kazi hii nilikuwa nalipwa mshahara wa Shs 280/= kwa mwezi na nilikuwa nimepita mtihani wa sheria, karatasi ya kwanza ya Somo la Mahakama za Mwanzo "PRIMARY COURTS".

## *PICHA NA VYETI VINGINE*

Picha 1 Ukurasa wa Kwanza wa mswada wa Maisha ni kugharimia .........75

Picha 2 Ukurasa wa Pili wa mswada wa Maisha ni kugharimia.................76

Picha 3 Ukurasa wa Tatu wa mswada wa Maisha ni kugharimia ...............77

Picha 4 Mnyampala Machichimi, baba mzazi wa Mathias E. Mnyampala 78

Picha 5 Mary Mangwela Mnyampala "Wastara", mke wa Mathias E. Mnyampala........................................................................................78

Picha 6 Mathias E. Mnyampala: Mwalimu wa Kiswahili katika Jeshi la Kujenga Nchi (J.K.T.) c.1960 ....................................................................79

Picha 7 Julius K. Nyerere na Mathias E. Mnyampala katikati ya Mkutano wa Washairi (1968) ...........................................................................79

Picha 8 Kaburi la Mathias E. Mnyampala – Dodoma (2007) .....................80

Picha 9 Ai ndwele yaniuma (Mvumi Hospital Dodoma - 7/3/69) ..............81

Picha 10 Msanii wa Taifa (1987) ..............................................................82

Picha 11 Nishani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1994)...............83




**Picha 1 Ukurasa wa Kwanza wa mswada wa Maisha ni kugharimia**

© MNYAMPALA 2013 (mswada na maandishi yake); © ROY 2013 (picha)



115

la "Maisha ni Kugharimia". Asili ya Kupewa jina hili Kuna maana Kamili. Utastaajabu sana ukisikia Kwamba mtungaji wa Kitabu hiki hakujaliwa Kupelekwa Shuleni na wazazi wake mpaka alipokwisha ~~K~~ balehe, na baada ya Kuozwa na Kulipa Kodi ya Serikali Kama vyeti viwili ndipo alipoanza Kusoma Shule za vijijini hata sasa amefaulu Kama watu wengine waliopata bahati ya Kupelekwa Shuleni na wazazi wao au jamaa zao. Hii ndio maana ya jina la Kitabu hiki Kuitwa "Maisha ni Kugharimia".

Duniani Kitu bora ni Kuwa na moyo mkuu. Watu wengine ~~wengine~~ hukata tamaa na Kurudia njiani. Kukata tamaa Kunamletea mtu Kufifia Kwa maisha yake. Jaribu-jaribu mpaka umeona umefaulu Kabisa. Ukishindwa usikate tamaa. Duniani hatukukaa Kwa raha ni taabu tu. Lazima Kushughulika siku zote tu za maisha yetu hapa duniani — Si mfalme Si tajiri, Si maskini ~~sa~~ fukarai siku zote maisha twashughulikia. Wewe ukisema labda Mfalme ndiye mwenye raha, la! maana halali usingizi upesi akifikiria namna ya Kuendesha nchi yake ili ipate Kustawi, au Kufikiri namna ya Kujiweka tayari iwapo itatokea mashambulio ya ghafla ya adui zake, na jinsi gani atende hata ashinde.. Kadhalika tajiri nae hufikiri sana jinsi ya Kuendeleza

**Picha 2 Ukurasa wa Pili wa mswada wa Maisha ni kugharimia**

© MNYAMPALA 2013 (mswada na maandishi yake); © ROY 2013 (picha)


116

Utajiri wake, au sivyo atapotewa na
Utajiri na kumjia umasikini ambao
utamletea hali mbaya. Mawazo hayo
huwaletea kukosekana kwa usingizi.
Na fukara vile vile namna ya kuchu-
ghulika ili apate riziki yake. Kwa
hiyo ulimwenguni "Maisha ni ku-
gharimia". Walimwengu husema "shida
ni mwalimu wa maarifa" ni kweli. Tena
Wanasema: "Ajizi ni nyumba ya njaa."
Basi usishindwe. Jaribu jaribu tu mpaka
uone mwisho wake. Nani ashikae
mundu na shoka kufyeka pori hata
ashike jembe kulima akakosa mavuno!
Taabu na mashaka ulimwenguni ndivyo
tulivyoahidiwa – bidii na jasho lofu ndi
raha yetu; na Elimu bila jitihada ku-
rudia ujiani na kushindwa mitihani.
Piga moyo konde kuendelea, hata ukim
mkubwa mpaka umefaulu ~~Kadiri~~ ya
Kabisa, au Kadiri yake.

**Picha 3 Ukurasa wa Tatu wa mswada wa Maisha ni kugharimia**

© MNYAMPALA 2013 (mswada na maandishi yake); © ROY 2013 (picha)



**Picha 4 Mnyampala Machichimi, baba mzazi wa Mathias E. Mnyampala**



**Picha 5 Mary Mangwela Mnyampala "Wastara", mke wa Mathias E. Mnyampala**




**Picha 6 Mathias E. Mnyampala: Mwalimu wa Kiswahili katika Jeshi la Kujenga Nchi (J.K.T.) c.1960**



**Picha 7 Julius K. Nyerere na Mathias E. Mnyampala katikati ya Mkutano wa Washairi (1968)**




**Picha 8 Kaburi la Mathias E. Mnyampala – Dodoma (2007)**

© ROY 2007



\- 2 -

6. Na mwezi Februari, haondoka Mzizima,
Mapema nikaabiri, nikaja zangu Dodoma,
Kidogo hapata heri, na chakula nikauma,
Ai Ndwele yaniuma, ~~nombeeni Washairi.~~ nawaarifu sahiba

7. Hewa naiona safi, kwa afya yangu ni njema
Japo afya bado ghafi, bali navuta mtima,
Najaribu vuta kafi, kwa maguu nachechema,
Ai ndwele yaniuma, ~~nombeeni Washairi~~ nawaarifu sahiba

8. Nipo Mvumi Spitali, ya Wilaya ya Dodoma
Najiona afadhali, naweza hata kusema,
Ninamwomba Jalali, anijalie uzima,
Ai ndwele yaniuma, ~~nombeeni Wash~~ nawaarifu sah

Mathias E. Mnyampala,
Mvumi Hospital
DODOMA.

7/3/69

**Picha 9 Ai ndwele yaniuma (Mvumi Hospital Dodoma - 7/3/69)**

© MNYAMPALA 2013 (waraka na maandishi yake); © ROY 2013 (picha)

Mathias E. Mnyampala anaendelea kuandika mashairi katika kijitabu wakati alilazwa Hospitali na kushikwa vibaya na ndwele. Beti tano za kwanza hazipatikani (mhariri).



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, UTAMADUNI,
VIJANA NA MICHEZO

TAMASHA LA KWANZA LA SANAA NA LUGHA YA TAIFA
DODOMA
2 OKTOBA 1987—6 OKTOBA

MSANII WA TAIFA

Ndugu Hayati Mathias Mnyampala

ametambuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ametunukiwa heshima ya kuwa MSANII WA TAIFA kwa uwezo na juhudi kubwa aliyoonyesha kwa maendeleo ya Sanaa na Lugha nchini katika fani ya Mashairi na ngonjera

Tarehe 6 - 10 - 1987

*Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Utamaduni, Vijana na Michezo*

**Picha 10 Msanii wa Taifa (1987)**

© ROY 2007 (picha)



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



NISHANI YA JAMHURI YA MUUNGANO

HAYATI MATHIAS MNYAMPALA ALIZALIWA HUKO DODOMA MWAKA 1919, NA KUFARIKI DUNIA MWAKA 1969. ALISOMA KATIKA SHULE YA MSINGI YA BIHAWANA MKOANI DODOMA.

MWAKA 1946 HADI 1960 ALIAJIRIWA SERIKALINI KAMA KARANI, AKIFANYIA KAZI HIYO HUKO MANYONI, KONGWA NA MPANDA. MWAKA 1960 HADI 1965 ALIKUWA HAKIMU WA MAHAKAMA YA MWANZO MPANDA. MWAKA 1965 ALIHAMISHIWA DAR ES SALAAM ALIKOENDELEA KUWA HAKIMU HADI MWAKA 1969, ALIPOFARIKI DUNIA. AMEZIKWA DODOMA.

HAYATI MATHIAS MNYAMPALA NI MTUNZI MAARUFU WA KISWAHILI. AMEANDIKA MAKALA MBALIMBALI KATIKA MAGAZETI NA AMEWAHI KUWA MTUNZI WA MASHAIRI YALIYOGHANIWA REDIONI. KATIKA UHAI WAKE AMEANDIKA VITABU 13 VILIVYOCHAPISHWA NA INASADIKIWA KUWA IPO MISWADA YAKE MINGI AMBAYO HAIJACHAPISHWA. MIONGONI MWA VITABU VYAKE MAARUFU NI DIWANI YA MNYAMPALA, VITO VYA HEKIMA, KISA CHA MRINA ASALI NA WENZAKE, NGONJERA ZA UKUTA, JUZUU I NA II, UMOJA NI NGOME YETU, NA HISTORIA, MILA NA DESTURI ZA WAGOGO.

HAYATI MATHIAS MNYAMPALA NI MWANDISHI MWANZILISHI WA NGOJERA NA ANAYO NAFASI YA PEKEE KATIKA FANI HIYO. FANI YA NGONJERA IMEENEA KWA HARAKA HAPA AFRIKA MASHARIKI. IMEKUWA NI NJIA MOJAWAPO YA KUELIMISHA UMMA KATIKA MAMBO MBALIMBALI YANAYOGUSA MAISHA YAO YA KILA SIKU. FANI HIYO INAYOTUMIKA SANA MASHULENI, KATIKA VYOMBO VYA HABARI NA KADHALIKA, IMEWEZA KUPENYA MPAKA VIJIJINI, NA KUVUKA MIPAKA HADI NCHI JIRANI. AIDHA, HAYATI MNYAMPALA NI MWANZILISHI WA TENZI ZA AINA YA 'MTIRIRIKO NA MSISITIZO'. JUHUDI ZAKE HIZI NI MCHANGO MKUBWA KWA TAIFA HILI NA ULIMWENGU KWA UJUMLA KATIKA KUKUZA LUGHA YA KISWAHILI.

KWA SABABU HIZO, MIMI ALI HASSAN MWINYI, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, NAMTUNUKIA HAYATI MATHIAS MNYAMPALA NISHANI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.

IMETOLEWA IKULU KWA MUHURI NA SAHIHI YANGU LEO TAREHE 9 DESEMBA, 1994.

RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**Picha 11 Nishani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1994)**

© ROY 2007 (picha)

9 791092 789027 >

Marehemu Mathias E. Mnyampala (1917 – †1969) aliandika habari za maisha yake wakati alipokuwa ameshaona kwamba anakomea mwisho wa uhai wake kutokana na kuumwa sana na ndwele miaka 1968-1969. Wakati huo alikuwa ameshakuza sana lugha ya Kiswahili kwa ufasaha wake wa kishairi na mambo mengine mengi pamoja yake vitabu vyake kuhusu historia ya Ugogo, siasa ya Ujamaa, dini na maisha ya wafu maarufu kama Mtemi Mazengo na Sheikh Kaluta Amri Abedi.

Kwa sababu kumbe alifanikiwa sana kutoka utoto wake katika machunga ya Ugogo, bila kujua kusoma wala kuandika hadi umri wa kuoa mke na kulipa kodi, mpaka ubingwa wa lugha ya Kiswahili na utungaji wa idadi ya vitabu inayozidi ishirini na tano akiwa anadhaniwa na wataalamu wa ushairi wa Kiswahili na washairi wenzake wenyewe kuwa malenga mmoja mkuu wa Karne iliyopita.

Alikuwa mzalendo mkubwa wa Taifa la Tanzania na alijitolea kabisa kueneza lugha yake Kiswahili maisha yake yote. Mchango wake Mathias E. Mnyampala kwa fasihi ya Kiswahili na Taifa lake ni tukufu, kadiri ya kupewa heshima kubwa ya Nishani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Rais Ali Hassan Mwinyi mwaka 1994.

Mswada huu ambapo marehemu Mathias E. Mnyampala anatusimulia habari za maisha yake binafsi ulibaki muda mrefu sana uliozidi miaka arobaini bila kupigwa chapa. Uligunduliwa mwaka 2007 mjini Dodoma na kupata kuhaririwa mwaka 2013. Kwa mara ya kwanza, toleo hili kutoka shirika la DL2A – Buluu Publishing (Ufaransa) linawapa wasomaji watukufu na wapenzi wa Kiswahili nafasi ya pekee ya kugundua maisha ya mzungupule huyo wa Kiswahili na fasihi yake.

ISBN 9791092789027

90000 >

9 791092 789027